

KUTHIBITISHA NENO LAKE



Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu. Mpendwa Baba wa Mbinguni, tunashukuru ya kwamba tuko hapa usiku wa leo. Sisi, tunashukuru ya kwamba tunajua Uwepo Wako uko hapa pamoja nasi. Sasa tunaomba ya kwamba utahudumia kila mmoja wetu, kadiri tunavyohitaji. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina. (Ketini.)

² Ninajisikia vizuri tu kuwa na maikrofoni hizi zinazofanya kazi. Nilisikitika sana kwa namna fulani ilivuruga mambo jana, ule Ujumbe niliotamani sana muupate.

³ Nami nilitaka muwe na hakika kuona jambo hilo. Ndiyo ninii—nanga tuliyo nayo. Sisi hatutui nanga katika kanisa. Tumetia nanga katika Kristo, unaona. Yeye pekee ndiye hiyo Njia. Yeye ndiye mahali pekee pa usalama, mahali pekee ambapo Mungu aliwahi kuweka Jina Lake. Na Mungu alisema angekutana na watu katika mahali alipopachagua kuweka Jina Lake; sio katika lango lolote, bali katika lango alilochagua. Na katika mahali hapo Yeye angekutana na watu, na hapo peke yake. Nasi tunaona ya kwamba Mungu hakuliweka Jina Lake mahali popote ila katika Mwanawe, Yesu Kristo, kwa kuwa mwana daima hulichukua jina la baba yake.

⁴ Na sasa wewe unasema, “Vema, hilo liko wapi siku hizi? Kila mtu anasema, ‘Mimi niko ndani ya Yesu.’”

⁵ Yeye ni Neno. Ambapo, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” Tena, imeandikwa pia katika Ufunuo mlango wa 19, tunapomwona Yeye akija, Bibi-arusi na Bwana Arusi, vazi Lake lililochovywa katika Damu, “Jina Lake aliitwa ‘Neno la Mungu.’” Yeye ni Neno la Mungu.

⁶ Na, hiyo ni kusema, Yeye ni nguvu za kuhuisha. Yeye huyo Roho Mtakatifu ndiye ile, da—dainamikia zinazolingia kwenye mitambo, hayo Maneno, yanayoifanya hiyo mitambo hai. Na kila sehemu inapaswa kutenda kazi kwa upatano, la sivyo haitafanya kazi hata kidogo. Inabidi kuchukua Biblia nzima, kumchukua Kristo mzima, kuchukua Injili yote.

⁷ Ninataka kuliambia, jopo hili nililoangalia kwenye televisheni jana usiku, nikijua ya kwamba litaonyeshwa, nami nililiangalia. Nataka kutoa maoni juu ya hawa ndugu, wale waliokuwa kwenye jopo lile, njia stadi jinsi gani ya kujibu maswali! Na mimi ni mkosoaji sana, mwajua, hata hivyo, bali hapakuwa na kitu cha kukosoa pale. Yalikuwa ni mambo ya kweli kabisa, nami niliweza kukubaliana nayo, asilimia mia moja. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Asanteni. Amina. Majibu hayo yalikuwa sahihi juu ya alama. Kwa kweli nilifurahia jambo

hilo. Laiti ningalikuwa na filamu ya kulionyesha kanisani mwangu huko nyumbani. Kwa kweli lilikuwa ni jambo zuri sana.

⁸ Nami ninashukuru sana kujua ya kwamba—ya kwamba Mungu ameshughulika katika zile milki zingine, mbali na kundi letu wenyewe la Kipentekoste, nasi tunawakusanya watu, ule uzao wa Mungu, ambao umekuwa huko nje miaka hii yote, ukingojea Nuru ile iwamulikie.

⁹ Na pia inatupa onyo, enyi wezangu, kujua ya kwamba Yesu alisema, “Wakati hawa wanawali waliolala walipoanza kuja kununua Mafuta, hapo ndipo Bwana Arusi alipokuwa anakuja.” Kwa hiyo tunaweza kuona kwa jambo hilo, tunapowaona Waespiskopalian, Wapresbiteri, Wamethodisti, Wabaptisti, Walutheri, wakija kununua Mafuta, basi hiyo ilikuwa ndiyo saa ambayo Bwana Arusi alikuja. Hebu na tukumbuke jambo hilo.

¹⁰ Kamwe Billy, mwanangu, hajapata kuniambia jambo kama lile aliloniambia muda mfupi tu uliopita. Alisema, “Baba, mimi sikwambii la kufanya. Simaanishi kukushawishi kwa cho chote, ila,” kasema, “baba, lo lote ufanyalo, weka wakati wako wote kwa ajili ya hao wagonjwa.” Akasema, “Sijapata kuona wagonjwa wengi jinsi hii!” Kasema, “Nilisambaza kadi mia mbili katika dakika moja tu ama mbili.” Kasema, “Kuna wagonjwa wengi sana!” Ni nadra sana yeye kuniambia jambo hilo.

¹¹ Na halafu nimekuja usiku wa leo nikiwa na mihtasari mifupi iliyoandikwa hapa, na maoni machache kuhusu hukumu ijayo, na nikijua ya kwamba tumeketi hapa usiku wa leo tukiwa tuna hasira ya Mungu ikitikisa chini yetu, na karibu italipuka. Basi tukijua ya kwamba hasira ya Mungu inangoja; katika muda ule tu itakapotamkwa, mambo yatakuwa yamekwisha, kwa mamilioni. Nami nikijua jambo hilo moyoni mwangu, na nikijua ya kwamba hivyo ndivyo itakavyokuwa! Na halafu tunaona wagonjwa wengi sana, wakisihia na kujitahidi.

¹² Nami nikawaza, “Usiku wa leo, wengi wao ni Wakristo.” Na hebu niseme haya, ninyi watoto wa Mungu. Lolote mfanyalo, achilieni kila kitu kengine kiende. Mtumikieni Mungu, mchana na usiku, kwa moyo wenu wote. Wewe, unaweza kuhisi kuna kitu fulani kasoro. Unaweza kujua hilo unapotembea mitaani, unaweza tu. . . na popote pale uendapo. Unajua, kama wewe ni wa kiroho; nami ninajua ninyi mu wa kiroho.

¹³ Nami nilikuwa nikizungumza na mtu mmoja, Ndugu Stromei. Sijui kama Tony yuko hapa, ama hayuko. Yeye, yeye alikuwa. . . [Ndugu fulani anasema, “Tony Salameh?”—Mh.] Tony Salameh, Salameh, Salameh? La. Sio huyo Tony. [Ndugu fulani anasema jambo fulani] La, huyo ni Tony mwingine. Huyu ni yule Tony wa huko—huko—huko Tucson. Jina lake ni nani? [Mtu

mwingine anasema, “Stromei.”] Stromei! Ninajua ni Salameh, Stromei, ama kitu fulani. Nimelipata . . .

¹⁴ Kwenye duka lake, hivi majuzi, kulikuwa na mtu fulani aliyeingia, ilikuwa ni ajabu sana, alikuwa akizungumza juu ya jambo fulani lililolikumbusha, wakati ni- . . . mara ya mwisho nilipokuwa huko—huko India.

¹⁵ Ambapo, nafikiri Bwana alitupa umati mkubwa sana tuliopata kuwa nao kwa wakati mmoja, ilikuwa huko Bombay. Hata hatungeweza kupata mahali popote pa kuwaweka, maelfu kumi na maelfu ya watu.

¹⁶ Na kabla tu hatujafika kule, kulikuwa na gazeti moja lililofasiriwa. Vema, ilikuwa, India ni nchi ya lugha mbili, lilikuwa—lilikuwa ni gazeti la Kiingereza. Nalo lilisema, “Vema, hapana budi matetemeko ya ardhi yamekwisha, ndege wanaruka kurudi nyumbani mwao kwenye viota vyao.”

¹⁷ Siku chache kabla ya hayo matetemeko kuja, ambayo yalibomoa nyua na kadhalika. Hao maskini ndege wadogo walijitafutia kimbilio miambani, na kujenga viota vyao; na alasiri ama adhuhuri, wakati jua ni kali sana, wanyama wote wanasimama kuzizunguka hizo kuta za miamba, kusudi wasimame kwenye kivuli. Na kwa siku mbili, hao ndege walikaa huko nje kwenye miti, wasingekuja kwenye viota vyao; na siku mbili, hao wanyama, kondoo na ng’ombe, wasingekaribia wakati wa alasiri, ama kukaa karibu na hizo kuta. Wali—walikaa huko nje kondeni na kuegemeana, wapate kivuli.

¹⁸ Ndipo ghafla, tetemeko la ardhi, ambalo lilitikisa tu hizo kuta na kuangusha majengo. Na, unaona, kama maskini ndege hao wadogo wangelikuwa pale, wangingamia. Kama ng’ombe wangelikuwa wamesimama chini yake, na hao kondoo, wangingamia. Mungu akiyaonya maumbile!

¹⁹ Siku chache zilizopita, huko chini katika duka la Ndugu Tony, nilikuwa nikimsikiliza mtu pale aliyesema . . . Wakati tetemeko hili lilipotukia huko Alaska, yeye alikuwa akivua samaki kule mahali tunapopaita Stony Point, huko Mexico. Naye akasema, “Ndege hawali, na samaki hawali. Kulikuwa na kasoro fulani. Ndipo, ghafla, tetemeko la ardhi likaanza.”

²⁰ Na hivi majuzi, wakati hilo lilipotukia kule India, ama popote pale lilipokuwa, alisema alikuwa akivua samaki tena. Naye akawaza, “Vema, ni ajabu. Hao samaki hula wakati kama huu. Hakuna mbingiriko hata mmoja majini, hakuna popote. Maji yametulia kabisa, wakati mzuri kabisa kwa samaki kula, bali hawakula. Na ndege wote ambao huwa huko nje kwa kawaida, shakwe, wanaokota samaki hawa na kadhalika, wote walikuwa wakitembea kila mahali huko ufukoni, wakisongamana pamoja. Katika muda mfupi, kuvumwani ya bahari kutoka chini ikaanza kupanda juu namna *hiyo*, tetemeko la ardhi lilikuwa limetukia upande wa pili wa

dunia.” Unaona, hao samaki walijua kulikuwa na kasoro fulani, jambo fulani lilikuwa karibu kutukia. Hao ndege walijua vivyo hivyo.

²¹ Hakika, kama Mungu humpa samaki na ndege utambuzi, ni zaidi sana vipi Yeye anapaswa kuwapa watoto Wa—Wake! Tunajua ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho, na hukumu inangoja, kwa hiyo hebu na tuwe na kicho sana. Mkimbilie Mungu kwa moyo wako wote! “Ee Kapernaumu, wewe uliyeinuliwa mpaka mbinguni, utashushwa mpaka kuzimu,” na leo uko chini ya kilindi cha maji. Hebu kumbukeni tu, na mwombe.

²² Sasa, usiku wa leo, ninataka kusoma mahali hapa katika Maandiko, kwa muda mfupi tu. Tutawaombea wagonjwa. Billy alisema alisambaza kitita cha kadi za maombi. Naye alisambaza baadhi jana, wala sijafikia yoyote ya hizo jana usiku. Nami nilishangaa, wakati Roho Mtakatifu alipokuja... Ni kwamba tu... Huwezi kumlazimisha atende kazi. Ni kama tu wenzo mdogo. Unajiingiza kwenye gia. Wewe ndiwe unayemtumia Roho Mtakatifu, si mimi. Unafanya hivyo wewe mwenyewe. Kwa hiyo mimi, jana usiku, niliona hata katika utambuzi, watu hawakuushika vizuri kabisa. Haikuonekana wanaushika. Niliona hilo, hapa hivi majuzi, inaonekana kana kwamba, takribani, wakati nilipokuwa nikizungumza, nikiwawekea wagonjwa mikono, wanajua.

²³ Tunapaswa kutambua ya kwamba ndani yetu tumepewa, sisi ambao tunamwamini Yesu Kristo na tumekwisha kuzaliwa kwa Roho Wake na kujazwa na hizo nguvu za kuhuisha, nguvu hizo zilizo ndani yenu. Kwa kuwekea mikono, juu ya wengine, kama vile wanafunzi walivyofanya na kote katika wakati, Hizo ziliwaponya kabisa wagonjwa, ziliwafufua wafu, zilionyesha maono, unabii. Na Roho yule aliyeishi miongoni mwa mitume wa hapo mwanzoni anaishi kanisani leo, akifanya mambo yale yale. Na upesi kama tunavyoweza kutambua jambo hilo! Unaona, haidhuru zinatenda kazi kiasi gani, inakubidi kutambua jambo hilo na kuliadini. Haitafaa kitu hata kidogo, mpaka uziamini. Lakini mara unapoziamini, shida zako zimekwisha. Hiyo ni kweli.

²⁴ Sasa hebu na tufungue kwenye Maandiko. Nilikuwa nimeketi huko nje, muda mfupi uliopita, nikaandika Maandiko mengine machache, ili kubadilisha somo langu kwa ajili ya usiku huu. Nami ninataka kusoma baadhi yake kutoka katika Neno la Mungu, kutoka katika Kitabu cha Luka Mtakatifu, mlango wa 8, kuanzia kifungu cha 40. Sikilizeni sasa, nitasoma kirefu.

Basi Yesu aliporudi mkutano ulimkaribisha kwa furaha, maana walikuwa wakimngojea wote.

25 Hivi hilo halingekuwa ni mkao mzuri kwa kundi hili usiku wa leo?

Na tazama, mtu mmoja akaja, jina lake Yairo, naye ni mtu mkuu wa sinagogi, akaanguka miguuni pa Yesu, akamsihi aingie nyumbani kwake;

Kwa kuwa binti yake yu katika kufa, ambaye ni mwana pekee, umri wake amepata miaka kumi na miwili. Na alipokuwa akienda makutano walimsonga.

Na mwanamke mmoja, ambaye ametokwa na damu muda wa miaka kumi na miwili, [aliyekuwa amegharimiwa mali zake zote kwa kuwapa waganga] asipate kuponywa na mtu ye yote,

Alikwenda nyuma yake, akaugusa upindo wa vazi lake; na mara hiyo kutoka damu kwake kulikoma.

Yesu akasema, Ni nani aliyenigusa? Basi, watu wote walipokana, Petro alimwambia, Bwana mkubwa, makutano haya wanakuzunguka na kukusonga, nawe wasema, Ni nani aliyenigusa?

. . . Yesu akasema, Mtu amenigusa, maana naona ya kuwa nguvu zimenitoka.

Yule mwanamke, alipoona ya kwamba hawezi kusitirika, akaja akitetemeka, akaanguka mbele yake, akamweleza mbele ya watu wote sababu yake ya kumgusa, na jinsi alivyoponywa mara.

Akamwambia Binti, jipe moyo: imani yako imekuponya; enenda zako na amani.

Alipokuwa akinena . . . , alikuja mtu fulani kutoka nyumbani kwa yule mkuu wa sinagogi, akamwambia, Binti yako amekwisha kufa; usimsumbue mwalimu.

Lakini Yesu aliposikia hayo, alimjibu, akasema, Usiwe na hofu, amini tu, naye ataponywa.

Alipofika nyumbani hakuacha mtu kuingia pamoja naye ila Petro, . . . Yakobo, na Yohana, na babaye yule mtoto na mamaye.

Na watu wote walikuwa wakilia . . . kumwombolezea; akasema, Msilie, hakufa huyu, bali amelala usingizi tu.

Wakamcheka sana, maana walijua ya kuwa amekwisha kufa.

Lakini akawatoa wote nje, akamshika mkono, akapaza sauti na kumwita huyo msichana, akisema, Kijana, inuka.

Roho yake ikamrejea, naye mara hiyo akasimama. Akaamuru apewe chakula.

Wazazi wake wakastaajabu sana, lakini akawakataza wasimwambie mtu lilitukia.

²⁶ Sasa na tuombe. Mpendwa Baba wa Mbinguni, tunaposoma Neno hili, tunajua ya kwamba jambo hilo ni kweli. Hili lilitukia. Si hadithi fulani ya kubuni tunayosoma labda kutoka katika gazeti fulani ama kitabu fulani cha hadithi za kubuniwa, lakini hili linatoka katika Kitabu ambacho tunajua kuwa ni Neno la Mungu. Tunaamini lilitukia. Tunaamini ya kwamba Yesu huyu aliyefanya jambo hili kuu, mara mbili hapa, la mwanamke aliyetokwa na damu, na mtoto aliyekufa, tunaamini ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu, ya kwamba Mungu alimfufua kutoka katika wafu naye amemleta kwetu, usiku wa leo, katika Utu wa Roho Mtakatifu.

²⁷ Nasi tunaamini ya kwamba Yeye yuko hapa pamoja nasi usiku wa leo. Na tunaamini ya kwamba ni Yeye yule jana, leo, na hata milele, huruma Zake zinawafikia watu. Na watu wanapomwendea, matokeo yale yale yaliyotolewa siku ile yatatolewa leo. Tujalie hayo tena, Baba, ili tupate kuwa na upako mpya. Kama vile Ndugu Shakarian alivyoomba kwa uaminifu sana, muda mfupi uliopita, na akaomba wasikilizaji waamini, tunaomba tena katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁸ Ninataka kuzungumza kwa muda kidogo tu, na huo utakuwa tu muda mfupi, maana ninataka kuwaleta hao watu walio na kadi za maombi hapa na kuwaombea. Na kuacha jambo lingine lolote ila tu kuwaombea wagonjwa. Lakini kabla ya kuwaombea wagonjwa, inatupasa kuwaweka watu katika mtazamo huo. Mtazamo ndio daima unaoleta matokeo. Ni mtazamo unaochukua kuhusu Mungu.

²⁹ Hapa kuna mwanamke aliyegusa vazi Lake, aliponywa, akitokwa na damu. Askari alimtemea mate usoni Mwake na kuweka taji la miiba kichwani Mwake, wala hakuhihi uwezo wowote.

³⁰ Ni jinsi unavyoliendea. Mtazamo ndio unaotakiwa. Na hivyo ndivyo ilivyo usiku wa leo, rafiki mpendwa, inatakiwa mtazamo. Sisi tuko, na tunaamini kwamba tuko, katika Uwepo wa Yesu Kristo, bali ni mtazamo wako ambao huleta matokeo. Mitambo iko hapa, na vivyo hivyo pia nguvu tendaji. Kama unaweza tu kuanza, Mungu atafanya yaliyosalia.

³¹ Sasa, somo hili ninalotaka kuzungumza juu yake, kwa muda kidogo, ni: *Kuthibitisha Neno Lake*. Sasa hilo ni jambo kubwa, kuliwazia: *Kuthibitisha Neno Lake*.

³² Sasa Mungu anaweza kabisa kuthibitisha Neno Lake, usiku huu, kama alivyowahi kulithibitisha. Na Biblia ilisema pia, "Thibitisheni mambo yote. Shikilia yaliyo mema."

³³ Sasa mmesikia, hapana shaka, mmesikia ile methali ya kale, "Lithibitisha, nitaliamini." Bali hilo si kweli. Mara nyingi nimeona mambo mengi yamethibitishwa, ambayo hata yalikuwa

yamethibitishwa kabisa kisayansi, na watu hawakuyaamini hata hivyo.

³⁴ Nilikuwa nikizungumza na mtu mmoja, hapa si muda mrefu uliopita. Tulikuwa tukizungumza juu ya uponyaji wa Kiungu. Alisema, “Mimi nisingeamini jambo hilo. Sijali nini kingetukia, ni thibitisho la kiasi gani ungeweza kuonyesha la jambo hilo, ningali siamini jambo hilo.” Vema, bila shaka, haidhuru ungemfanyia nini mtu huyo, yeye—yeye amepotea. Hawezi kuamini. Hakuna kitu chochote ndani yake, cha kuamini.

³⁵ Nilikuwa tu na tu—tukio dogo hapa, kama juma moja lililopita, kama vile nyote mjuavyo ya kwamba mimi—mimi huwinda. Na niliporudi kutoka kwenye mkutano wangu, nilikuwa nikiwinda simba. Na baada ya kuhamia Arizona, ni kuzuri, ninapenda kuwinda wanyama wakubwa, pia ninapenda kutoka nje niingie katika maumbile na kuyaangalia.

³⁶ Sasa, mimi si mwuaji. Ninawinda tu. Kwa hiyo, si—sipendi kuangamiza wanyama pori, si—sidhani ni vizuri. Nafikiri ni dhambi tu kuua wanyama pori, wakati huwali na unaenda kuwatumia kwa kusudi fulani, kama vile ingekuwa kuua kitu kingine cho chote. Ninaamini ni makosa. Hatupaswi kufanya hivyo. Mungu alitupa hao kwa ajili ya chakula na kwa makusudi mbalimbali, wala hatupaswi kuwaangamiza. Lakini sasa wale sheria inaosema unaweza kuwachukua, ni sawa. Ila tu usiwe mharibifu.

³⁷ Nami nikiwa kule chini, msimu wa vitu vingine vyote umeanza. Simba wanawaua ng’ombe wengi. Nami ninawajua wenye ranchi wengi huko mashambani. Na kila wakati wanapoua mmoja, mbona, wananiita, wakati simba anapoingia miongoni mwa kondoo. Rafiki yangu fulani, hivi majuzi usiku, alipoteza kama dola elfu tatu mia tano, katika usiku mmoja, kwa simba mmoja akiwaua tu wana-kondoo. Aliingia, na, bila shaka, hao simba wengine lazima watalipia dhambi yake. Na kwa hiyo nikamwua huyo simba, na kwa hiyo alikuwa ni simba mkubwa mno, na mwenye urefu wa futi tisa, na alikuwa na uzito wa karibu mbili na kitu, kwa hiyo alikuwa—alikuwa simba mkubwa mno.

³⁸ Na halafu nikatoka katika nchi ya Arizona, nikaenda huko Utah, kuwinda. Na kwa hiyo niliambiwa ya kwamba kulikuwa na watu kule, ya kwamba mtu niliyekuwa nikienda kuwinda naye, alikuwa ni mtega wanyama wa serikali, “Na, jamani, usitaje lolote kuhusu dini, ukiwa karibu naye.” Kasema, “Yeye kweli alikuwa ni mtu mkali sana.”

³⁹ Nami nikasema, vema, nilimwambia mtu niliyekuwa nikienda naye, nikasema, “Sitaitaja.”

⁴⁰ Akasema, “Usiseme, ‘mhubiri.’ Ukisema, kamwe hutaenda kuwinda. Hatakuchukua.” Kasema, “Niliwinda pamoja naye siku tatu, na nikalala pamoja naye kila usiku, nikala naye

kila siku, wala hata hakusema, ‘Habari za asubuhi. U hali gani? Unataka kitu cha kula? Osha vyombo.’ Hakuongea kitu!” Kasema, “Sasa usiseme jambo lolote kuhusu jambo hilo.”

⁴¹ Nikasema, “Sitasema neno.” Kwa hiyo sikumwambia sitaomba, lakini niliendelea tu kumwambia ya kwamba mimi ni... Nami naomba.

⁴² Kwa hiyo tulipofika kule, mtu huyo alikuwa mgumu sana, wala sikuamini yeye aliamini lolote. Naye alikuwa amepoteza mtoto mchanga siku chache zilizopita usiku, mtoto aliyezaliwa mfu. Kwa hiyo, tukaenda kuwinda. Na siku ya pili, mtu yule niliye kuwa nikiwinda naye alikuwa amemwambia, alimwambia mimi huwinda kila mahali nchini. Kwa hiyo wakati yule mwindaji mwingine, aliyekuwa pamoja nami, alipoondoka, tulikuwa huko juu ya vilele kabisa; ambako ndiyo kwanza tumfukuze simba, mpaka tukamwingiza kwenye miamba, naye alikuwa ametoroka. Na kwa hiyo tulikuwa tumeketi pale tukiingojea mbwa arudi. Ndipo mtu huyu akaniambia, akasema, “Yule mwindaji mwingine, rafiki yako, ananiambia ya kwamba unaenda kuwinda kila mahali. Hivi una pesa nyingi sana?” Kasema, “Mimi nadhani hilo halinihusu.”

⁴³ Nami nikasema, “La,” nikasema, “sio fedha nyingi sana.” Nikasema, “Ni—ninadhaminiwa.”

⁴⁴ Ndipo akasema, “Loo, kumbe.” Akasema, “Vema, nadhani hilo halinihusu tena, lakini,” kasema, “je! una shirika fulani linalokudhamini?”

⁴⁵ Yeye alikuwa anavuta maneno kutoka kwangu. Nili ahidi sitaninii, unaona. Kwa hiyo nikasema, naam, nikasema, “La, bwana. Mimi ni mhubiri, mmishenari.”

Akasema, “Ati nini?”

⁴⁶ Nikasema, “Mmishenari.” Ndipo akasimama tu na kuniangalia kwa dakika chache.

⁴⁷ Nikasema, “Je! una matumaini yoyote kwa Maisha ya baadaye? Tumaini lako ni nini?”

Akasema, “Mimi ni Jack Mormon.”

Nami nikasema, “Ati nini?”

Akasema, “Jack Mormon.”

Nikasema, “Ni aina gani hiyo?”

⁴⁸ Kasema, “Ile inayotukana na kunywa kahawa, na kuvuta sigara.”

Nikasema, “Vema, ungamo aminifu ni zuri kwa ajili ya nafsi.”

⁴⁹ Basi akasema—akasema, “Ninataka kukuuliza jambo fulani.” Akasema, “Nasikia ya kwamba kanisa la Mormon ndilo kanisa la kweli peke yake lililopo.” Akasema, “Je! unaamini jambo hilo?”

50 Nikasema, “Inapofikia suala la kanisa, nadhani ni zuri tu kama lolote la hayo. Ninajua tu Ukweli mmoja, na huyo ni Yesu Kristo.” Nikasema, “Ninajua Yeye ni Kweli.”

51 “Vema,” akasema, “nilikuwa na mtoto mchanga aliyezaliwa hivi majuzi usiku, akiwa mfu.” Akasema, “Ninasikia ya kwamba mtoto huyu mchanga, kwa sababu alizaliwa mfu, Mungu kamwe hakumpulizia pumzi ya uhai ndani yake, kwamba sitamwona tena kamwe.” Akasema, “Je! unawazia nini juu ya jambo hilo?”

52 “Vema,” nikasema, “Hutamwona ukiwa Jack Mmormon, hakika hutamwona. Hilo ni jambo moja la hakika, hutamwona almradi tu unadumu kuwa Jack Mmormon.” Naye akasema... Vema, alikuwa akinichimba niongee, kwa hiyo nami nikamchimba kurudi nyuma kidogo, unaona. Tulikuwa—tulikuwa na wakati wa kuchimbana. Kwa hiyo akasema—akasema... Nikasema, “Kuna nini?”

Akasema, “Loo, sijui.” Kisha akasema, “Vema, unafikirije?”

Nikasema, “Ninawajua ninii wengi wazuri...”

53 Sikujua alikuwa Mmormon. Nami nilikuwa ni ninii sana... Ninajua, nikiwa huko Utah, labda ilikuwa, bali mimi... maana watu wengi kule ni Wamormon, kuzunguka mji wa Salt Lake. Hapa hapakuwa mji wa Salt Lake, hata hivyo. Kwa hiyo nikawazia, “Vema, nimekuwa na baadhi ya marafiki kadha wazuri wa Mormon, wamekuwa kwenye mstari wa maombi, watu wazuri.”

54 Ndipo nikasema, “Nimekutana na watu wazuri sana ambao ni—ni Wamormon.” Naye akasema, vema, akasema... Nikasema, “Sijui fundisho lao juu ya jambo hilo, wala nisingetaka kusema jambo lolote dhidi ya mafundisho yao, kwa sababu hicho ndicho ulicho, nami ninaheshimu jambo hilo sana.” Kisha nikasema, “Vema, nawe unaamini jambo hilo?”

Akasema, “Naam, bwana, ninaamini. Lakini,” kasema, “Siliishi.”

55 Nikasema, “Vema, ninaamini ya kwamba Biblia inafundisha ya kwamba Mungu alimjua mtoto huyo mchanga, mamilioni ya miaka iliyopita, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Nikasema, “Mungu alimwambia Yereima, ‘Kabla hujazaliwa kamwe katika tumbo la mama yako, kabla hujatoka tumboni, nalikujua, nalikutakasa, na kukuweka kuwa nabii kwa mataifa.’” Nikasema, “Hicho ndicho kiasi alichojua juu yake, unaona.”

Akasema, “Vema,” akasema, “asante.”

56 Akaanza kushuka kilimani. Na ndipo akakutana na jamaa huyu mwingine, naye akasema, “Kwa nini hukuniambia ya kwamba jamaa huyo alikuwa mhubiri?” Na kwa hiyo tukaninii... Akazungumza naye kidogo na kuanza kumwambia juu ya mikutano.

57 Sasa, Wamormon wanaamini unabii. Mimi sininii . . . huenda kusiwe na yeyote hapa, bali wao wanaamini katika—katika unabii. Lakini, kwa hiyo, labda ninazungumza kielimu, bali mimi. . . Naam. Naam. Lakini, hata hivyo, wanaamini.

58 Naye anasema, akarudi kwangu, akasema, “Ninasikia ya kwamba wewe ni nabii.”

59 Nikasema, “La, bwana.” Nikasema, “Mimi . . . Bwana amenionyesha mambo machache yatakayotukia.”

60 Ndipo akaondoka, mara moja, kasema, “Hebu tuingie ndani.” Ndipo akaingia kwenye gari lake, akashuka akaenda kwa . . . Kulikuwa na mji mdogo kutoka mahali alipoishi. Katika dakika chache, hakuwako. Tulikuwa tukiwatayarisha mbwa, twende kuwinda tena mara baada ya chakula cha mchana. Na tulipofanya hivyo, mbona, akaondoka kwa gari lake.

61 Katika dakika chache, kijana mwenye sura nzuri akarudi, mwenye umri wa kama miaka kumi na saba, Mkristo mwungana aliyeonekana mcha Mungu sana. Akasema, “Huyu ni ndugu yangu.” Kasema, “Yeye si Jack Mormon. Yeye ni Mmormon halisi.”

Nikasema, “U hali gani, mwanangu?”

62 Naye akasema, “Nasikia, ya kwamba ndugu yangu ananiambia, ya kwamba wewe ni nabii.”

63 Nikasema, “La, bwana.” Nikasema, “Si kwamba mimi ni nabii.” Nikasema, “Bwana amenionyesha mambo yatakayotukia.”

64 Akasema, “Nina sindano mkononi mwangu sasa hivi, ninapaswa kuwa nimelazwa juu ya meza ya upasuaji.” Akasema, “Lakini ndugu yangu aliniambia jambo hili. Nami nikasema, ‘Kama hivyo ndivyo ilivyo, sihitaji upasuaji.’” Akaniangalia moja kwa moja jichoni, mtazamo mwaminifu, wa kweli na mnyofu, akasema, “Weka mikono yako juu yangu. Kama mambo haya ni kweli, sitahitaji upasuaji.” Akaenda nyumbani akiwa mzima.

65 Ndugu huyu, rafiki yangu Mkristo, alikuwa akiwinda pamoja nami, kutoka Phoenix. Akaniambia, akasema . . . Baadhi ya vijana hawa wameketi papa hapa sasa. Mmoja wao ninajua yuko hapa. Tukaenda nyumbani. Akasema, “Ndugu Branham, kama Bwana angekuonyesha ono na akuwezeshe kuwaambia hao Wamormon yale hasa yatakayotukia, hilo litatosha, kwa kuwa wanatazamia jambo hilo.”

66 Kwa hiyo, niliomba na kuomba. Na nilipokuwa nikirudi nyumbani, nilikuwa nikija, Jumatatu iliyofuata, Jumapili, yapata saa nne, nilikuwa nimesimama chumbani, baada ya kuhudhuria kanisani asubuhi hiyo, nami nilikuwa nikiangalia nje.

⁶⁷ Nami nikaona vimulimuli vikimulika, ama namna fulani ya nuru ikimulika. Nami nikaona simba aliyekuwa kwenye mti, na—na alikuwa ni mdogo mno kwangu mimi kumpiga risasi. Sikutaka kufanya hivyo. Na kulikuwa na mtu mwingine aliyempiga risasi, na, walipofanya hivyo, walimpiga risasi kwa bunduki kubwa kupita kiasi. Ikamrarua yule simba. Sikufurahishwa na vi—vi—vile ilivyofanywa.

⁶⁸ Nilipofika huko Phoenix, nilimwambia Ndugu Dawson jambo hilo, na Ndugu Mosley. Ninajua yuko hapa. Nilimwona hivi majuzi, mahali fulani hapa. Naye alikuwa akiambatana nami, yeye na mke wake. Ndipo nikasema, “Angalieni na mwone, hilo ni BWANA ASEMA HIVI. Itatukia namna hiyo.”

⁶⁹ Usiku mwingi tulingoja, usiku nne ama tano, tulikuwa tumewinda, ama kwa siku nyingi. Ni shida sana kumkimbizia simba apande mtini usiku. Ilitukia kwamba, walipokuwa wakija nyumbani, waliwafungulia mbwa, mwindaji huyu, mvulana huyu Mmormon. Ndipo huyo si—simba akashika harufu, ama mbwa akashika harufu ya simba, hasa, na kumfukuza akapanda mtini. Na saa nne usiku walikuja, wakatuamsha toka usingizini. Tulitoka tukaenda kule, na hapo alikuwapo simba yule yule juu ya mti. Akiwa anammulika tochi, Ndugu Mosley alimpiga risasi kwa bunduki yenye kipenyo cha arobaini na nne, karibu imlipue huyo simba nusu vipande viwili. Na hivyo ndivyo, jinsi ilivyokuwa imenenwa hasa.

⁷⁰ Kesho yake, nilikutana na bwana nyama mkubwa wa jimbo hilo, Jack Mormon mwingine. Nikawachukua vijana hao pamoja, nikawaongoza nyumbani kumrudia Kristo.

⁷¹ Nawaambia, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mungu huthibitisha Neno Lake kwamba ndivyo lilivyo.

⁷² Mmewasikia watu wakisema, “Kuona ni kuamini.” Kwa jumla hilo si kweli. Watu wengi huona wala hawaamini.

⁷³ Zile siku Yesu alipokuwa duniani, kwa nini hawakumtambua, kwamba Yeye alikuwa ni hilo Neno la Mungu lililodhihirishwa? Kwa nini watu hawakutambua ya kwamba Musa alisema, “Bwana Mungu wako atawaondokesha nabii mithili Yangu”? Naye alitimiza kila Neno ambalo Biblia ilisema kwamba angefanya, bali hawakuamini jambo hilo.

⁷⁴ Lakini Mungu, katika kila kizazi, amethibitisha Neno Lake kuwa la kweli. Yeye daima hulithibitisha Neno Lake. Ndipo mara nyingi wao husema, ya kwamba, “Kuona ni kuamini.” Sivyo ilivyo. Lakini tunajua ya kwamba Mungu huenda moja kwa moja akilithibitisha Neno Lake katika kila kizazi.

⁷⁵ Tunajua ya kwamba Yeye aliwathibitishia Adamu na Hawa, ya kwamba wakati aliposema, “Siku mtakayokula, siku hiyo hakika mtakufa.” Hatuna budi kulikubali, ya kwamba ni kweli. Tunaliamini, kwa maana Yeye ametuthibitishia hilo, na tunajua ya kwamba ni kweli.

⁷⁶ Sasa tutachukua tu sehemu kadhaa ambapo Mungu alithibitisha Neno Lake. Hebu na tuchukue, kwa mfano, katika siku za—za Nuhu. Mungu alisema na Nuhu ujumbe ambao bila shaka ulikuwa usio wa kisayansi na usioaminika. Hakuna mtu angaliweza kuamini. Haijawahi kunyesha juu ya nchi. Sio kisayansi!

⁷⁷ Labda wao walikuwa kizazi kikuu cha kisayansi kutuliko sisi sasa, kwa maana walijenga mapiramidi na masifinksi, na kadhalika, katika siku hizo, ambayo sasa hatuwezi kujenga. Walikuwa wanajua nguvu fulani, za namna fulani za nguvu za mitambo, labda za atomiki ama cho chote kile, ambapo wangepoteza kuinua majabali hayo makubwa, ambayo tusingeweza leo kuyainua. Lakini walifanya mambo makuu ya kisayansi. Walikuwa na kitu fulani ambapo wangepoteza maiti, kuifanya ionekane ya kawaida kwa mamia ya miaka. Tumepoteza ustadi huo.

⁷⁸ Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Nasi tunajua ya kwamba inabidi tuingie katika wakati mwingine mkuu wa kisayansi.

⁷⁹ Na sasa ujumbe aliokuwa nao Nuhu ulikuwa ni kinyume sana na imani ya siku hiyo, katika kanisa, na pia ulikuwa ni wa kinyume kabisa cha utafiti wa sayansi. Lakini Mungu alithibitisha Neno Lake kuwa la kweli. Mungu alithibitisha ya kwamba yale huyo nabii alisema yalikuwa kweli.

⁸⁰ Pia tutamchukua mwingine kwa muda kidogo tu. Ibrahimu alikuwa ni nabii mwingine wa Bwana, ambaye alijiliwa na Neno. Na kumwambia, wakati alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, na Sara alikuwa na miaka sitini na mitano, ya kwamba atampata mtoto kwa Sara. Sasa, hilo lilikuwa ni mshtuko kwa asiyeamini. Hivi ungeweza kuamini, leo, jambo kama hilo likitukia hata katika siku hii, pamoja na mafanikio yetu yote ya kisayansi, na watoto hawa wote wa maabara wanaosema habari zao, na kadhalika? Lakini mwanamke huyu bikizee, sasa mwenye umri wa miaka sitini na mitano, na mzee wa miaka sabini na mitano, lakini Neno la Bwana lilimjia Ibrahimu na kumwambia ya kwamba jambo hili litatukia. Naye Ibrahimu akamwamini Mungu. Sasa, haidhuru Mungu alisema mara ngapi, na jinsi ilivyokuwa ni kweli, ilimbidi Ibrahimu kuamini yale Mungu aliyosema, kulifanya litimie. Sasa angalia jinsi mtu huyo alivyojaribiwa, akiwa na ushuhuda wake, kwamba kweli aliamini.

⁸¹ Mtu yuyo huyo aliyekiri hivyo, ya kwamba alimwamini Mungu, yeye ni mtu kama ulivyo wewe, unayeketi hapa usiku wa leo. Tungali tunamwamini Mungu. Inatupasa kuamini ya kwamba Neno Lake ni Kweli. Naye atalithibitisha, ya kwamba ni Kweli, kama tu tutaliamini.

⁸² Sasa angalia vipingamizi alivyokuwa navyo Ibrahimu. Jambo la kwanza lilikuwa ni umri wake, umri wa miaka sabini na tano, naye Sara akiwa na sitini na tano. Alikuwa amepita sana badiliko la maisha, kukatika hedhi. Hapana shaka kwamba ilikatika, miaka mingi huko nyuma. Yeye alikuwa amekwisha ishi naye kama mke. Alikuwa ni dada yake wa kambo, huenda alikuwa amemchukua wakati alipokuwa msichana tu katika utineja wake, naye alikuwa amemwoa. Na yeye hakuwa amepata watoto. Mkewe alikuwa tasa kabisa. Na sasa tunaona ya kwamba, ili afanye jambo hili, ilimbidi kujitenga na watu wote ambao hawakuamini jambo hilo, kulifanya litimie.

⁸³ Simaanishi kusema inakupasa kujitenga na watu. Bali inakubidi kujitenga na umbeya wote wa kutokuamini, na ukae mbali nao. Watu wanaposema, “Aha, mambo hayo hayatukii! Hilo ni kundi la wendawazimu! Hakuna kitu kama hicho kinachotendeka,” ziba tu maskio yako na uondoke. Usisikilize jambo hilo.

⁸⁴ Biblia ilisema ya kwamba “Ibrahimu hakisita katika ahadi ya Mungu, kwa kutokuamini; bali alikuwa na nguvu, akimsifu Mungu.” Jina lake lilibadilishwa kutoka Abramu kuwa Ibrahimu, kubadilishwa kwa jina kulilifanya jina lake, “baba wa mataifa.” Ungeweza kuwazia mtu akiishi na mkewe, mpenzi wake, ambaye alikuwa ameishi naye sasa kwa miaka hii yote, na sasa mahali fulani katika umri wa miaka themanini, na mke wake umri wa miaka sabini, na hata hivyo bila mtoto mmoja wala tumaini lolote la mtoto, hata hivyo akadai kwamba alikuwa ni “baba wa taifa.” Ungeweza kuwazia ukosoaji wa wanaume wenzake waliokuwa wakipita wangesema, “Wewe Baba wa mataifa, sasa una watoto wangapi wakati huu?” Na ukosoaji wote uliombidi kupitia!

⁸⁵ Bali Ibrahimu hakisita mahali popote hata kidogo, kwa kutokuamini. Yeye aliamini ya kwamba Mungu aliweza kutimiza yale aliyokuwa ameahidi, ya kwamba Mungu angehibitisha Neno Lake, haidhuru ilichukua muda mrefu jinsi gani. Lakini badala ya kuendelea kuwa mnyonge kila wakati, kama vile tulivyozoelea kufanya, aliendelea kuzidi kupata nguvu sikuzote. “Kama halikutukia leo, kesho itakuwa ni muujiza mkubwa zaidi, maana limekaa siku moja zaidi.” Huyo alikuwa ni Mungu, huyo alikuwa ni Mungu katika Ibrahimu, kwa kuwa alijua ya kwamba Mungu alithibitisha Maneno Yake yote kwamba ndivyo yalivyo.

⁸⁶ Ikiwa watoto Wake watalichukua tu Neno Lake, kusudi apate kulithibitisha kupitia kwako! Hivyo ndivyo tu anavyoweza kuthibitisha Neno Lake.

⁸⁷ Yeye halithibitishi kwa wasioamini. Hawawezi kuthibitishiwa; wao ni wasioamini. Lakini, Hilo si kwa wasioamini. Si kwa ajili ya wasioamini.

⁸⁸ Ni kwa yeye aaminiye. Na kama Yeye anaweza kumpata mtu ambaye ataliamini Neno Lake, Yeye atalithibitisha Neno Lake kwako. Na mara nyingine magonjwa na kadhalika hutupata kwa njia hiyo, kwamba Mungu aweze kujithibitisha Mwenyewe.

⁸⁹ Je! unamkumbuka yule kipofu ambaye Yesu alimkuta? Wao walisema, “Ni nani aliyetenda dhambi, yeye ama baba yake, mama yake?”

⁹⁰ Akasema, “Katika jambo hili, si ye yote wao, bali ni kwamba kazi za Mungu zipate kujulikana.” Unaona, ilitendeka kwa mvulana huyo kusudi Yesu apate kutukuzwa. Wakati mwingine ugonjwa si laana, ni baraka, tupate kudhihirisha imani yetu kule nje na kuita vitu hivyo visivyo, kana kwamba vilikuwapo. Mungu alisema hivyo, na Yeye atalithibitisha jinsi hiyo kama tu hutadhoofika chini ya hilo jaribio.

⁹¹ Yeye aliweza kumthibitisha Ayubu, wakati mmoja, kwamba asingeweza kumlaani mbele Zake. Hebu angalia jaribio ambalo Ayubu alilipitia. Lakini huko ndani chini kwenye taya zenyewe za mauti, yeye hata hivyo alisema, “Bwana alitoa, Bwana ametwaa, Jina la Bwana litukuzwe!” Yeye bila shaka aliliamini jambo hilo. Mungu alithibitisha Neno Lake kwa Ayubu. Alilithibitisha kwa Ibrahimu. Alilithibitisha kwamba ndivyo lilivyo.

⁹² Pia alilithibitisha kwa Musa. Na wakati Musa, wakati shida ilipokuwa imembana sana, Musa alikuwa akiwazia moyoni mwake, ya kwamba labda, kuwa mkombozi, ya kwamba mama yake alikuwa labda amemwambia alikuwa amezaliwa mtoto mzuri. Yeye—Yeye alikuwa ndiye mwalimu wake ambaye alimlea katika jumba la kifalme la Farao, bila shaka alikuwa amemwambia, “Mwanangu, tumeomba ya kwamba tutakombolewa, nasi tunaamini ya kwamba wewe ndiye mtoto yule ambaye Mungu atamtumia kukomboa.” Na ndipo wakati aliponinii . . .

⁹³ Unaona, yeye alikuja naye alikuwa awe mwa—mwana wa binti Farao, na tunaona ya kwamba alikuwa awe mrithi wa kiti cha enzi. Mbona, si ajabu ni jambo lililokuwa niani mwao wakati huo, ya kwamba angekuwa halifa wa Farao, “Na hivyo ndivyo ambavyo angaliwakomboa hao watu, kwa yeye kuwa halifa wa Farao.” Bali Mungu alikuwa na . . . Kama jambo hilo lingalikuwa hivyo, basi angalilifanya kupitia mambo ya mwilini, kupitia te—te—tendo la kisiasa. Lakini Mungu hatendi kazi jinsi hiyo kila mara.

⁹⁴ Mungu ana njia Zake mwenyewe za kufanya kazi, Naye alisema “angewatoa.” Alimwambia Ibrahimu, “Baada ya miaka mia nne,” Yeye, “angewatoa, kwa mkono wenye nguvu,” angewaonyesha “ishara na maajabu.” Kwa hivyo hangeweza kufanya jambo hilo jinsi hiyo, kwa hiyo Ibra- . . . Tunaona ya

kwamba Ibrahimu alimwamini Mungu, naye huyu hapa Musa akimwamini Mungu.

⁹⁵ Na Musa aliangalia kupitia kwenye dirisha lile lile ambalo Farao aliangalilia, aliona watu wale wale. Huyu Farao aliwaangalia, kama “Watu waliolaaniwa, watu wasiokuwa na kitu ila lundo la ushupavu wa dini, kwa ajili ya Mungu fulani, na Mungu fulani wa jangwani mahali fulani ambaye hawakujua kitu juu Yake; nguzo fulani isiyoonekana ambayo wanaomba, ambayo haikuwa cho chote. Wao ni kundi la washupavu wa dini. Nao walikuwa ni kundi la watumwa. Na Mungu wao akiwaacha wawe watumwa, ilitibitisha ya kwamba Yeye hakuwa Mungu.”

⁹⁶ Na katikati kabisa ya jambo hilo lote, Yeye alikuwa akimwinua mtu yule yule. Mungu hufanya mambo kwa njia za kipekee sana, papo hapo chini yao. Si mwanatheolojia, si mwalimu, si kuhani, si mmoja wa watu wao watakatifu; bali ni mtu wa kawaida tu, aliyezaliwa kwa ajili ya kazi hiyo. Na Mungu akamwita apate kuwa nabii Wake, na akamtuma kule. Na bila kitu mkononi mwake ila fimbo iliyopindika, kukabiliana na jeshi, vikosi vya magari vilivyokuwa vimeushinda ulimwengu mzima. Lakini akiwa na fimbo hiyo mkononi mwake, kama vile Mungu alivyomwambia ashike fimbo hiyo mkononi mwake naye angewakomboa Israeli, naye akashuka akaenda akafanya hivyo kwa maana Mungu aliliahidi. Atafanyaje jambo hilo? “Nitakuwa pamoja nawe.”

⁹⁷ Akasema, “Nionyeshe utukufu Wako, Bwana. Mimi ni mzito wa kunena. Siwezi kuzungumza vizuri. Na ni- . . .” Alikuwa na visingizio milioni moja.

⁹⁸ Bali Yeye alisema, “Nitakuwa pamoja nawe.” Na hilo tu ndilo lililohitajika. Alienda, akilichukua Neno la Mungu. Haidhuru lilionekana kuwa ni jukumu la hatari jinsi gani, Musa aliendelea kumwamini Mungu. Naye Mungu akathibitisha Neno Lake, kupitia kwa Musa, kuwa ni kweli. Kwa sababu, haidhuru ni jambo gani lililotukia, Musa alidumu moja kwa moja na Neno. Katika wakati wa ile safari. . .

⁹⁹ Mungu aliwaambia, kule Misri, pia, ya kwamba angewakomboa, “Kuingia katika nchi ya ahadi, nchi nzuri, iliyojaa maziwa na asali.” Na ilikuwako kweli kabisa. Wao hawakujua ilikuwako, bali Yeye alisema, “Iko, Nami nimewapa ninyi. Ni yenu tayari, enendeni mkaidai tu!”

¹⁰⁰ Na huko jangwani, wakati wengi wao walipotoka, wakicheza katika Roho, wakati Miriamu alipocheza tari; wakila mana kutoka Mbinguni; wakamsikiliza Musa akiimba katika Roho; wakiiangalia muujiza na ishara zikitendeka. Lakini ilipofikia shindano la kuamua, kuamini Neno lote la Mungu, ahadi yote, walishindwa.

101 Ni wawili wao tu ndio walioliamini, hao walikuwa ni Yoshua na Kalebu. Nao walirudisha ushahidi ya kwamba nchi hiyo ilikuwa nzuri.

102 Lakini, hali ya mambo ilivyokuwa, hilo ndilo lililowazulia. Kwa sababu, walisema, “Hatuwezi kuiteka nchi hiyo, kwa maana miji yao imezungushiwa kuta, wa—wa—wawakilishi wao kule. Si wawakilishi wao, bali wa—watu wao ni majitu makubwa mno. Mbona, tunaonekana kama panzi, tukilinganishwa nao.”

103 Yoshua na Kalebu wakasema, “Sisi tunaweza hata na zaidi kuiteka.” Kwa nini? Mungu alikuwa amewapa hiyo nchi, haidhuru majitu hao walikuwa ni wakubwa jinsi gani. Kizuizi hicho hakikumaanisha kitu kwao. Mungu alikuwa amesema hivyo! Na Mungu alilithibitisha jambo hilo kupitia kwao. Nao kweli walienda wakaiteka nchi, kama vile Mungu alivyosema wangefanya. Aliwathibitisha jambo hilo.

104 Sasa, walipokuja katika mwezi wa Aprili, wakati maji yalipokuwa yakiruka kutoka milimani, juu ya vyungu vya theluji, na kadhalika, na ikaonekana kana kwamba Mungu alikuwa jemadari duni, kuliongoza jeshi Lake moja kwa moja hadi mahali fulani, alipowafanya wabanwe wasiingie kwenye nchi ya ahadi. Na wakati ule ule aliowavusha, alipokuwa akienda kuwavusha, ulikuwa ndio mwezi mbaya sana katika mwaka. Ule mwezi ambao Yordani ilikuwa ikifurika, ilienda mpaka mashambani. Mbona, kama walikuwa wakienda kuwavusha, ingekuwa ni katika msimu wa kiangazi, wakati ambapo wanaligeza kuvuka kupitia majini. Lakini Yeye alingoja mpaka maji yalipokuwa na kilindi. Yeye hupenda kujionyesha ya kwamba Yeye ni Mungu. Yeye hupenda kuthibitisha Neno Lake, haidhuru hali ikoje.

105 Sijali kama daktari alisema, “Wewe unakufa kwa kansa.” Hilo tu ndilo mtu huyo analojua. Labda maji yana kilindi kwa baadhi yenu, usiku wa leo. Lakini, kumbukeni, Mungu alifanya ahadi. Mungu hutimiza Neno Lake, na Mungu huthibitisha Neno Lake. Ni kweli.

106 Alingoja mpaka maji yalipokuwa yamejaa matope, mpaka yalipopata kilindi na yakawa juu ya vichwa vyao, na kadhalika, ndipo akafungua njia. Yeye aliwatangulia na kufanya njia.

107 Wataingiaje, hiyo Yeriko, wakati yote ilikuwa imefungwa? Yoshua alikuwa anashangaa. Alijua Mungu alikuwa amemwongoza umbali huo, hatua inayofuatia ni ya Mungu.

108 Siku moja, wakati alipokuwa huko nje akitembea, akiziangalia kuta, alimwona Mtu mmoja amesimama amechomoa upanga Wake. Na yeye akachomoa upanga wake na akaenda kumkabili Mtu huyo, akasema, “Uko upande wa nani Wewe? Je! uko pamoja nasi ama Wewe uko upande wa adui yetu?”

¹⁰⁹ Yeye akasema, “Mimi ni Jemadari wa majeshi ya Bwana.” Naye akamwambia la kufanya. Atapigaje tarumbeta na ukuta uanguke, ambapo wangeweza kuendesha mashindano ya magari ya farasi juu yake? Huo ungekuwa na uhusiano gani na tarumbeta?

¹¹⁰ Mungu hutumia njia rahisi kama hizo. Ndivyo ilivyo, urahisi wake, ndicho kinachomfanya Mungu kwangu mimi. Daima tunajaribu kupata vitu fulani vikubwa, vitakavyofanya jambo fulani, naye Mungu. . . shirika fulani kubwa litakalochukua kitu hicho chote na kukifagilia mbali. Wakati, Mungu huchukua mtu wa kawaida, mtu mmoja tu ambaye Yeye anaweza kumshika mikononi Mwake, Naye atathibitisha kila Neno alilosema, kwa Neno kwake. Inahitaji njia rahisi kama hizo!

¹¹¹ “Piga tarumbeta.” Si kuchimbua huo ukuta, ila, “Piga tu tarumbeta, na kuta hizo zitaanguka chini. Sauti ya tarumbeta itazianguka kuta hizo.” Ni jambo la kipumbavu jinsi gani kwa fikara za kimwili! Lakini Mungu alithibitisha Neno Lake lilikuwa kweli, kwa kuwa hizo kuta zilianguka, mmoja juu ya mwingine. Walienda moja kwa moja na kuuteka mji huo.

¹¹² Loo, Mungu hupenda kujithibitisha kwamba Yeye ni Mungu! Yoshua alijua jambo hilo. Siku moja, na wakati alipokuwa amesimama pale, moja ya vitendawili vikubwa sana vilivyowahi kutukia, nje ya kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu Kristo. Wakati adui. . . Alipokuwa amewashinda, na majeshi mbalimbali yalikuwa milimani. Alikuwa amewashinda kabisa, na jua lilikuwa likishuka. Loo, jamani, ulikuwa ni wakati wa jinsi gani kwa Jemadari Yoshua!

¹¹³ Kumbuka, yeye aliipiga nchi hiyo nzima, bila ya kuwa na hospitali, nesi, kikosi cha huduma ya kwanza, wala mtu aliyejeruhiwa. Niambie kitu kinachoweza kushinda hilo. Naam, bwana. Kamwe hakuwa na hospitali, hakuna manesi, wala hakumpoteza mtu yeyote, ilimradi tu walitembea katika mapenzi na Neno la Bwana. Mungu alithibitisha ya kwamba alikuwa yu pamoja nao. Hiyo ni kweli. Angalia sasa.

¹¹⁴ Nasi tunaona ya kwamba Yoshua alijua, kama usiku ukiingia, wangepenya na kuungana pamoja, na—na kuunganika na kufanya jeshi lingine kubwa, naye angekuwa na wakati mgumu nao kesho yake. Hakujua la kufanya, kwa hiyo alimtegemea Mungu. Alihitaji msaada, naye alihitaji hilo jua lisimame kimya. Kwa hiyo yeye aliamuru tu hilo jua lisimame kimya, na ninii. . . akasema na “mwezi ning’inia juu ya Aiyaloni,” wala visisogee mpaka atakapoviamuru. Ndipo mwezi na jua vikasimama kimya kwa muda wa saa ishirini na nne, wakati Yoshua alipompiga vita na kumshinda adui, kwa maana alikuwa moja kwa moja kwenye wajibu wa kazi. Alikuwa na haki ya kufanya hivyo, kwa maana alikuwa akitii amri ya Mungu.

¹¹⁵ Na alimuradi tu uko kazini, ukilitimiza Neno la Mungu, ukifanya yale tu Yeye aliyokwambia ufanye, ukitembea kwa maagizo ya Mungu, una haki ya kuuambia mlima huo, “Ng’oka!”

¹¹⁶ Mungu hutimiza Neno Lake. “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ usitie shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba hilo ulilosema litatimia, hayo uliyosema yatakuwa yako.” Yesu alisema hivyo, katika Marko 11:22. Hiyo ni Kweli. Ninajua hiyo ni Kweli. Ni Neno la Mungu, na hiyo inathibitisha kwamba ni Kweli. Tunahofu tu wakati mwingine. Tunafikia mahali, tunahofu hatatimiza Neno hilo. Yeye atatimiza Neno hilo. Yeye alisema atafanya hivyo. Sasa, tunaona jambo hilo ni kweli. Yeye alilithibitisha.

¹¹⁷ Unabii wa Isaya, wakati mmoja, ambao ni jambo ambalo halijawahi kamwe kutukia; halijawahi kutukia tangu hapo awali, wala halijatukia tangu wakati huo. Yeye alisema, “Bikira atachukua mimba.” Ungeweza kuwazia mwanamke, bila ya kumjua mwanamume, angepata mtoto? Isaya alisema, “Bikira atachukua mimba.”

¹¹⁸ Naye Mungu alimsababisha bikira kuchukua mimba, kuthibitisha Neno Lake kwamba ni kweli. Yeye alithibitisha Neno Lake, maana bikira kweli alichukua mimba na akamzaa huyo Mwana.

¹¹⁹ Sasa, Neno hilo lililofanyika mwili, angalia vile lilivyofanya. Wakati huyo Mwana alipozaliwa, Yeye alikuwa Neno Mwenyewe. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.”

¹²⁰ Yeye alikuwa ni hilo Neno lililo hai. Alithibitisha alikuwa Neno hilo lililo hai. Yeye aliwaambia hao waalimu wa siku hiyo, “Ni nani anayeweza kunihukumu mimi kwamba nina dhambi?” *Dhambi* ni “kutokuamini.” “Ni nani anayeweza kuniambia ya kwamba Mimi ni asiyeamini? Kila Neno lililoandikwa juu Yangu, limetimizwa.” Bashiri saba za mwisho za maisha Yake zilitimizwa katika saa saba za mwisho, msalabani. Kila kilichoandikwa juu Yake, kilitimizwa, kwa sababu Yeye alikuwa Neno. Yeye alithibitisha angalikuwa, alikuwa. Aliwaponya wagonjwa. Aliwafufua wafu. Alishinda mauti, kuzimu, na kaburi. Yeye alithibitisha alikuwa Neno.

¹²¹ Angalia kisa hiki hapa katika nyumba ya Yairo. Yeye alikuwa... Alikuwa amewaambia kweli. Tunamwona wakati akivuka bahari. Anaingia.

¹²² Kulikuwa na maskini mwanamke mdogo juu ya kilima, aliyekuwa ametumia pesa zake zote kwa waganga. Hapana shaka, waganga walikuwa wamefanya yote waliyojua kufanya, wapate kumponya mwanamke huyo; labda ni waganga wa Kiebrania, na huyo alikuwa ni mwanamke Mwebrania, kwa hiyo

walikuwa wamefanya yote waliyoweza kumfanyia dada yao. Ingawa, hawakuwa na cho chote cha kukomesha kutokwa huku na damu, ambako kulikuwa, labda, wakati wa kukatika hedhi na damu yake ilikuwa imetoka mpaka yeye. . . maskini jamaa huyo alikuwa mdhaifu sana ilikuwa ni vigumu kwake kutembea tena. Naye alikuwa amesikia kuhusu Yesu. Na wakati alipoona maskini kile chombo kidogo kikiingia kwenye miti ya majini, alishuka akaenda kule apate habari.

¹²³ Wakosoaji wake wengi sana walikuwa wamesimama pale. Wala Yeye hakosi wakosoaji leo. Kama wangelijua kwamba Yeye alikuwa ni Nani, wasingalikuwa wakosoaji Wake. Bali walikuwa wakosoaji Wake kwa kuwa hawakujua Yeye alikuwa ni Nani.

¹²⁴ Na hivyo ndivyo ilivyo na Ujumbe leo, wanaume wengi wazuri sana na wanawake wanaukusoa Huu kwa maana hawajui ni Kitu gani.

¹²⁵ Yesu alisema, “Kama mngalimjua Musa, mngalinijua Mimi. Musa alinena habari Zangu. Watu wengi wakuu walitamani kuiona siku hii. Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Nina ushahidi mkubwa zaidi,” akasema, “kuliko ule wa Yohana, kwa kuwa kazi nizifanyazo Mimi, zinathibitisha ya kwamba Baba yuko pamoja na Mimi.” Yeye alikuwa na kazi kuu zaidi, kwa kuwa alikuwa yule Aliyetambulishwa. Yohana alitambulishwa pia, kama sauti ya mtu aliaye nyikani. Lakini wakati alipokuja, Yeye alikuwa Ndiye Yule nabii ambaye Musa alikuwa amesema angeinuliwa.

¹²⁶ Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, Yeye alikuja katika majina matatu; jina la Mwana wa Mungu, Mwana wa Adamu, na Mwana wa Daudi.

¹²⁷ Wakati alipokuwa hapa duniani, mara ya kwanza, Yeye alikuwa ni Mwana wa Adamu. Asingekuwa Mwana wa Mungu wakati huo; hakudai kuwa hivyo kamwe. Yeye alisema alikuwa ni “Mwana wa Adamu.” Wakati mtu ye yote angemhoji, Yeye alisema, “Mnamwona Mwana wa Adamu; Mwana wa Adamu.” Sasa, “Mwana wa Adamu” ni *nabii*. Ilimbidi aje namna hiyo, kwa sababu, Maandiko, Yeye hawezi kuja kinyume cha Maandiko.

¹²⁸ Hiyo ndiyo sababu, siku hizi, kwamba Ujumbe we—wetu wa wakati huu hauwezi kuja kupitia kwa wanateolojia na theolojia, unapaswa kurudi kwenye kitu kile kile ulichoahidi kufanya. Hauna budi kuwa hivyo.

¹²⁹ Kwa hiyo tunaona ya kwamba, katika Mtu huyu, ilibidi awe nabii. Si Mwana wa Mungu pale, ilibidi Yeye awe Mwana wa Adamu. Yehova Mwenyewe aliwaita manabii, Yeremia na hao wengine, “Mwana wa Adamu.” “Mtakapomwona Mwana wa Adamu. . .” “Ni nani Mwana wa Adamu,” walishikilia kuuliza.

¹³⁰ Ndipo, alitumikia wadhifa Wake kama Mwana wa Adamu. Kisha akatekeleza wadhifa wake wakati huo kama Mwana

wa Mungu. Mungu ni Roho, na wakati huu sasa alipotumika katika Nyakati za Kanisa, kama Mwana wa Mungu. Sasa, katika Utawala wa Miaka Elfu, Yeye atakuwa ni Mwana wa Daudi, hapo atakapoketi kwenye kiti cha enzi cha Daudi. Atakuwa mrithi wa kiti hicho cha enzi, Mwana wa Daudi. Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu, Mwana wa Daudi, na ni Mtu yule yule daima.

¹³¹ Ni kama vile tu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu; wadhifa wa Mungu. Yeye alikuwa ni Mungu Baba, kisha akawa Mungu Mwana, sasa Yeye ni Mungu Roho Mtakatifu. Si Miungu watatu; Mungu mmoja, madhihirisho matatu, sifa tatu za Mungu yule yule.

¹³² Sasa tunaona, na katika saa hii tunayoishi sasa hivi, Mungu hudumu na Neno Lake jinsi tu alivyofanya wakati ule uliopita.

¹³³ Tunaona ya kwamba alivuka bahari. Mwanamke huyu alimwamini, kulikuwa na kitu fulani ndani yake kilichoanza kupigapiga kwa nguvu. Hakuwa na Maandiko kwa ajili ya jambo hilo, si Maandiko zaidi kuliko aliyokuwa nayo Yohana ya kulisimamisha jua, bali aliamini moyoni mwake ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Kwa hiyo akasema, "Laiti ningaliweza kugusa vazi Lake, nitaponywa." Kwa hiyo akapenya kupitia kwenye umati wa watu mpaka akaligusa vazi Lake, na kule kutoka damu kukakoma.

¹³⁴ Sasa, Yeye akawaangalia wasikilizaji, apate kujua ni nani aliyemgusa. Hapana shaka, kulikuwa na mtu fulani. Akasimama. Watu wote wakimsonga; na wengine wakimtania, wengine wakimchekelea; makuhani wakisimama kwa mbali na kumhoji maswali, na makasisi, na kadhalika. Lakini kulikuwa na wengine waliomwamini. Na, na muda si muda akasimama, kwa ghafla, akageuka, akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

¹³⁵ Baadhi yao walisema, "Mbona, Bwana!" Ninaamini Petro ndiye aliyesema, "Mbona, umati wote unakusonga. Mbona, ni nani 'aliyekugusa?' Mbona, kila mtu anakugusa!"

¹³⁶ Yeye akasema, "Lakini ninaona nguvu zimenitoka." Alijisikia mdhaifu. Ulikuwa ni mguso wa aina tofauti.

¹³⁷ Laiti tungaliweza kuona jambo hilo, ndugu, dada! Laiti uangaliweza kumgusa kwa mguso huo wa hakika! Loo, enyi wagonjwa, ninajiandaa kuwaombea, katika dakika chache tu. Ninaamini ya kwamba nina Roho Mtakatifu, si Roho Mtakatifu zaidi ya mliye naye papo hapo mlipo, watu hawa waliye naye hapa. Roho Mtakatifu yule yule, bali ni amri ya Mungu; na kama utaamini hiyo kuwa amri ya Mungu, ya kuwaombea wagonjwa, na kuwawekea mikono, na kutoa pepo wachafu, na ahadi ambazo amefanya, litakuwa ni jambo lile lile nawe. Utapata kile ulichoomba, kama unaweza kuamini.

"Je! unaweza kuamini ya kwamba mimi ninaweza kufanya jambo hili?" Yesu alisema.

¹³⁸ “Naam, Bwana, ninaamini,” alisema mtu yule aliyekuwa na mtoto aliyekuwa na kifafa, “Ninaamini ya kwamba Wewe ni Yule Mwana wa Mungu aliyekuwa aje ulimwenguni.” Sasa, tunajua ya kwamba hilo linaweza tu kuchukua mtazamo huo kuleta matokeo.

¹³⁹ Sasa, upesi, hebu na tuwazie habari Zake kwa muda kidogo, huyu hapa akipanda kwenda Zake barabarani. Maskini kuhani mmoja alishuka akaja, hapana shaka maskini mtu huyo alikuwa ni mwamini mkwamia mpakani.

¹⁴⁰ Wako wengi sana wao duniani siku hizi, maskini waamini wakwamia mpakani. Wanataka kuamini jambo Hilo. Wanataka kuamini ya kwamba Roho Mtakatifu ni halisi. Wanataka kuamini ya kwamba huu ni uamsho wa kimitume, kama Mungu alivyoahidi katika siku za mwisho angemmwaga Roho Wake. Sisi...anataka kuamini Malaki 4, ya kwamba Yeye aliahidi, katika siku za mwisho Imani ya a—asili ya kipentekoste ingerudishwa kwa—kwa kanisa tena.

¹⁴¹ Malaki 4 inadaid jambo hilo. “Angalieni, nitawapelekea Eliya katika siku ya mwisho,” hiyo ni kweli, “naye atawarudishia watoto Imani ya baba zao tena,” unaona, “Imani ya baba iwarudie watoto wao, pia.” Unaona, haina budi kutukia.

Unasema, “Vema, huyo alikuwa ni Yohana Mbatizaji.” La, la.

¹⁴² Yohana Mbatizaji alikuwa ni Malaki 3. Hiyo ni kweli. Mathayo 11 inasema hivyo, “Kama mnaweza kulipokea, huyu ndiye aliyenenwa habari zake, ‘Tazama, ninamtuma Mjumba Wangu mbele za uso Wangu.’” Ilikuwa ni Eliya, bila shaka. Yesu alisema alikuwa ndiye. Bali si Eliya wa Malaki 4, hata kidogo.

¹⁴³ Kwa sababu, “Mara baada ya Ujumbe huo, dunia itateketezwa kwa moto, na wenye haki watatembea juu ya majivu ya waovu.” Kwa hiyo halikutendeka katika wakati wa Yohana. Inatupasa kuwa na Ujumbe utakaosambaa tena na kuwatoa watu kutoka katika hali hizi zote za kimadhehebu, kuwarudisha kwenye Imani ya mwanzoni, halisi ya kipentekoste. Na tunaona jambo hilo likitendeka, ni kutimizwa kwa Maandiko ambayo hayana budi kutimizwa. Maandiko yote hayana budi kutimizwa. Ni mangapi zaidi ya hayo tungeweza kunena, ingenichukua zaidi ya wakati wangu uliokwisha sasa, kuwaonyesha. Lakini mnafahamu mambo haya, ya kwamba hayana budi kutukia barabara kabisa namna hii, kwa watoto wa Ibrahimu, kama tu vile Yeye alivyoahidi.

¹⁴⁴ Tunamwona Yesu akipanda kwenda sasa kumponya maskini yule msichana mdogo. Maana, baba yake, yule maskini mwamini mkwamia mpakani, jambo fulani lilifikia kiwango ambacho ilimbidi kumtambua Yesu, kwa hiyo, daktari alikuwa amemkatia tamaa. Ndipo akavaa maskini kofia yake nyeusi na akashuka kwenda kuona kama angeweza kumpata Yesu.

Unaona, Yeye daima yuko papo hapo wakati unampohitaji. Alimpata tu akija ufukoni.

¹⁴⁵ Ndipo akasema, “Njoo kwa msichana wangu mdogo, weka mikono Yako juu yake, naye atapona.” Kasema, “Yeye yuko karibu na kufa. Yeye ni mtoto wangu wa pekee.” Kasema, “Ana umri wa miaka kumi na miwili. Hatuna watoto wengine. Mke wangu pamoja na mimi,” labda, “tunazeeka. Na huyu ndiye mtoto wa pekee tuliye naye, naye yuko karibu na kufa. Bwana, ninakuamini. Kama tu utakuja na kuweka mikono Yako juu yake, atakuwa mzima.”

¹⁴⁶ Unaona, yeye alitambua nini? Alitambua ya kwamba lile Neno la Mungu lililoahidiwa lilikuwa limedhihirishwa katika Mtu huyu.

¹⁴⁷ Ni kama tu vile Nikodemo alivyosema, “Rabi, mwalimu, tunajua Wewe ni mwalimu utokaye kwa Mungu. Tunajua jambo hilo. Mafarisayo wanajua jambo hilo.” Kwa nini hawakukiri hilo? “Hakuna mtu angaliweza kufanya mambo ufanyayo, Mungu asipokuwa pamoja Naye. Tunajua ya kwamba Wewe umetoka kwa Mungu.”

¹⁴⁸ Hapa tunaona ya kwamba Yairo aliamini jambo lile lile. Yeye alisema, “Njoo uweke mkono wako.” Alijua ya kwamba Mungu alikuwa ndani Yake. “Weka mikono yako juu ya mtoto wangu. Ingawa yuko karibu na kufa, ataishi.”

¹⁴⁹ Alitembea tu pamoja naye. Na wakati alipokuwa akienda, huyu hapa mkimbaji anarudi, na kusema, “Usimsumbue, usimsumbue Bwana tena. Yule—yule msichana, amekufa, ameaga dunia sasa. Amefariki.”

¹⁵⁰ Yesu akamgeukia Yairo, akasema, “Je! sikukwambia, ‘Kama utaamini tu, utaona utukufu wa Mungu?’ Kama tu utaamini hayo!”

¹⁵¹ Akaingia chumbani, na hao hapo, wote wakupiga mayowe na kulia na kuomboleza, kama vile tu mtu yeyote angefanya. Maskini msichana mdogo mzuri, binti ya mchungaji, alikuwa amekufa, naye ameondolewa ulimwenguni humu. Na labda alikuwa amekwisha kufa kwa saa kadha, na halafu walikuwa wamemweka nje kwenye kitanda cha wagonjwa, na walikuwa tayari kuutia mwili wake dawa usioze, labda, na kumwondoa, na kisha mazishi.

¹⁵² Basi tunaona ya kwamba Yesu aliingia hapo nyumbani. Wote walikuwa wakilia kwa huzuni. Yeye anasema, “Tulieni.” Akasema, “Yeye hajafa, bali amelala.”

¹⁵³ Sasa ungeweza kufikiri waliyowazia? “Mbona, mtu huyu tunajua, sasa. Tunaelewa ya kwamba Yeye ni mtoto haramu. Na tunasikia juu ya ninii Yake, ubashiri Wake wote wa kipuzi anaobashiri. Na sasa tunajua ya kwamba kuhani anasema kweli, ‘mtu huyu ana wazimu,’ kwa kuwa tunajua ya kwamba

amekufa. Daktari alitangaza kwamba ‘amekufa,’ naye yule pale amelazwa. Ameaga dunia, nasi tunajua ya kwamba amekufa.” Wao wakasema, walimchekelea sana, kwa maneno mengine, walimfanya afadhaike, kwa kumkosoa.

¹⁵⁴ Lakini alikwisha kusema ya kwamba hakuwa amekufa. Hilo tu ndilo linalotakiwa. “Amelala.” Haidhuru kuna upinzani jinsi gani, Yeye atalithibitisha Neno Lake! Aliwatoa wote nje ya nyumba, akawaondoa wasioamini wote. Akamchukua Petro, Yakobo, na Yohana, waaminio, mashahidi watatu, na baba na mama, akaingia na kumshika huyo binti mkono, na akazungumza katika lugha iliyoiita nafsi yake irudi kutoka mahali fulani huko katika Umilele. Naye msichana huyo akaishi.

¹⁵⁵ Yeye alifanya nini? Alithibitisha Neno Lake. Alithibitisha kile alichosema. Hakuwa amekufa. Alikuwa amelala. Sasa tunaona, kufanya jambo hili, kutambua, Naye alithibitisha jambo lingine pale. Sasa alithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa Mungu. Alithibitisha ya kwamba Yeye aliyajua kabla hayajatukia. Angalia vile Neno Lake lilivyosema sasa. “Yeye hakufa, bali amelala.” Unaona, hakuwa amekufa, jambo la kwanza. Alikuwa amelala. Ilionyesha kutangulia Kwake kujua mambo. Sasa, huenda kulikuwa na maskini wasichana wengi wadogo waliokufa asubuhi hiyo hiyo, bali huyu hakuwa amekufa. Alikuwa amelala, kama vile Lazaro alivyokuwa. Naye akamwita kutoka katika usingizi huo, kwa kuwa hakuwa amekufa.

¹⁵⁶ “Naye aniaminiye Mimi, asijakufa, hata hivyo ataishi; na kila aishiye na kuniamini Mimi, hatakufa kamwe.” Ni wale tu walio kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, ambao aliwakomboa hapo alipokufa, hao ndio atakaowaita kutoka katika usingizi huo, kwenye siku hiyo, hao waliohuishwa na nguvu Zake, wale walio na hiyo nguvu ya kuhuisha iliyo ndani yao. Kama hata nilivyosema jana usiku; hata baada ya Eliya kufa, na mifupa yake ilikuwa iko kaburini, nguvu hiyo ya kuhuisha ilikuwa ingali iko kwenye mifupa yake.

¹⁵⁷ Hakika, Yeye alithibitisha kwamba Yeye alikuwa ni nani. Sasa tunaona tena, vivyo hivyo, Yeye alithibitisha pia, ya kwamba, katika Waebrania mlango wa 4 na kifungu cha 12, Yeye alithibitisha alikuwa ni Neno la Mungu. Hakika alithibitisha. Angalia alilofanya. Waebrania, 12, Waebrania 4:12 inasema ya kwamba, “Neno la Mungu lina nguvu zaidi, li jepesi zaidi kuliko upanga ukatao kuwili, na—na Huyatambua pia mawazo na makusudi ya moyo.” Angalia kwa muda kidogo sasa.

¹⁵⁸ Wakati alipoanza huduma Yake kwa mara ya kwanza, baada ya Yeye kutoka kuja kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Neno, wakati alipotoka jangwani kutoka katika majaribu Yake, kulikuwa na mtu aliyelitwa Petro, jina lake wakati huo lilikuwa

ni Simoni. Naye alikuja kwa Yesu akiwa pamoja na Ndugu yake, Andrea. Na mara tu alipoenda akaingia katika Uwepo wa Yesu Kristo, Yesu alisema, “Jina lako ni Simoni. Na la baba yako lilikuwa ni Yona. Tangu sasa utaitwa Petro.” Hilo lilithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni lile Neno, kwa maana Neno ni Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo. Yeye alikuwa Neno.

¹⁵⁹ Filipo aliona jambo hili likitukia. Akaondoka akaenda nyuma ya mlima, alikuwa amesafiri kwa siku moja, kisha akarudi. Naye alikuja na rafiki yake aliyeitwa Nathanaeli. Ndipo akasema, “Mambo haya kweli yanatukia. Musa alisema ‘Bwana Mungu wetu atatuondokeshea Nabii’ mithili yake, na huyu hapa Mtu huyo. Mbona, Yeye alimwambia Simoni kwamba alikuwa ni nani, hata kwamba baba yake alikuwa ni nani, nasi tunajua ya kwamba yale asemayo ni kweli. Kwa sababu, Mungu alisema jambo hilo katika Neno, na hapa imethibitika kwamba alikuwa afanye jambo hilo, na hilo linathibitisha ya kwamba huyo ndiye Masihi.”

¹⁶⁰ Ndipo wakati alipofika katika Uwepo Wake, Yesu alimwambia, akasema, “Tazama Mwisraeli, ndani yake hamna hila.”

¹⁶¹ Yeye akasema, “Rabi, ulinijua lini?”

¹⁶² Kasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona.” Yeye alithibitisha Neno Lake. Alithibitisha Neno la Mungu. Alilithibitisha.

¹⁶³ Yule mwanamke kisimani, wakati aliponinii . . . Vema, Yeye alimwomba ampe maji Anywe kutoka katika gudulia alilokuwa akichotea maji kutoka kisimani, naye akasema, “Si kawaida kweni Wayahudi kutuomba sisi wanawake wa Samaria kitu kama hicho, kwa kuwa hatuna uhusiano.”

¹⁶⁴ Akasema, “Lakini kama ungalijua ni nani uliyekuwa ukisema naye, ungaliniomba Mimi maji unywe.”

Akasema, “Kisima ni kirefu.”

¹⁶⁵ Na maongezi, yalipoendelea, hatimaye aliona shida yake ilikuwa ni nini. Naye akasema, “Nenda kamwite mume wako, na mje hapa.”

Akasema, “Sina mume yeyote.”

¹⁶⁶ Akasema, “Umesema kweli, kwa maana umekuwa na watano, naye uliye naye sasa siye mume wako.”

¹⁶⁷ “Mbona,” akasema, “bwana, naona kwamba Wewe ni nabii.” Akaninii . . . “Hatukuwa na mmoja kwa muda wa miaka mia nne, unajua.” Kasema, “Naona kwamba Wewe ni nabii. Sasa, tunajua ya kwamba Masihi ajapo, aitwaye Kristo, atakapokuja, atatwambia mambo kama haya. Hiyo itakuwa ndiyo ishara Yake.”

¹⁶⁸ Wakati aliposema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye,” Yeye alithibitisha Neno Lake. Yeye...sisi tunathibitisha kile alichodai kuwa. Yeye alikuwa Masihi, Mwana wa Mungu.

¹⁶⁹ Sasa tunaona, pia, ya kwamba maskini mwanamke huyu aliyekuwa na ugonjwa huu wa kutokwa na damu, aliyegusa vazi Lake, hilo pia lilimthibitishia yule ya kwamba Yeye alikuwa Ndiye Neno la Mungu.

¹⁷⁰ Sasa kumbukeni, usiku wa leo, Yesu alisema... Pia, katika Waebrania 1, Waebrania mlango wa 3, ninaamini ndipo, Yeye alisema ya kwamba, “Yeye sasa ni Kuhani Mkuu,” wakati huu tunaoishi sasa, “Kuhani Mkuu anayeketi katika Ukuu wa Mungu, huko Mbinguni, anayeweza kuchukuliana nasi katika mambo ya udhaifu wetu.”

¹⁷¹ Waebrania 13:8 ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Ni Mungu yule yule jinsi alivyokuwa wakati huo. Ni yeye yule usiku huu.

¹⁷² Yohana Mtakatifu 14:12, Yeye alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nifizanyazo mimi, yeye naye atazifanya. Hata nyingi zaidi ya hizi atazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu.” Unaona? “Yeye aniaminiye Mimi, kazi hizi nifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.

¹⁷³ Katika Mathayo 28, Yeye alisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari.”

¹⁷⁴ Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye anasimama, usiku wa leo, kulithibitisha Neno Lake. (Muda wangu umekwisha.) Lakini Yeye alithibitisha ya kwamba angeweza. Alithibitisha Neno Lake wakati huo, yale aliyokuwa ameahidi kwa wakati huo. Yeye aliyathibitisha maneno ya Isaya. Alithibitisha maneno ya Nuhu. Alithibitisha maneno ya Musa. Alithibitisha kila mojawapo ya maneno ya manabii.

¹⁷⁵ Yeye aliahidi ya kwamba katika siku hii, siku tunayoishi, kwamba ulimwengu utakuwa katika hali ya Sodoma, walawiti. Angalia tu jambo hilo ulimwenguni siku hizi, kila mahali ulimwenguni ninakosafiri; sio hapa tu, kila mahali. Ni jambo zito sana. Huko Sweden, vijana wanaume kwa wanawake huenda kuteleza kwenye theluji, uchi wa mnyama. Na huko Ujerumani na katika Ufaransa, na kwingineko kote, kwa namna fulani ni kama tu wahuni tulio nao hapa Marekani. Ni wakati wake. Mimi, endapo nitapata nafasi ya kurudi kamwe, ningependa kuzungumzia baadhi ya mambo ya kinabii, kwenu, na kuwaonyesha huo, wakati ambao tunaishi. Biblia ilisema ya kwamba, “Watoto watawatawala wazazi wao.”

¹⁷⁶ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... Neno.

¹⁷⁷ Lakini, kumbukeni, Ibrahimu alikuwa na uzao, ambao ulikuwa ni uzao wa Isaka. Alikuwa na wazao wengine baada

ya kifo cha Sara. Naye alikuwa na umri wa miaka mia moja na arobaini na tano, akamwoa mwanamke mwingine, akapata wana saba mbali na mabinti, maana Mungu alikuwa amembadilisha akawa kijana mwanamume wakati alipokuwa na umri wa miaka mia moja. Wakati huo alikuwa na yapata umri wa miaka arobaini na tano, kwa hiyo basi yeye... Tunajua jambo hilo. Nimewahubiria jambo hilo tu hapa California, miaka kadha iliyopita.

¹⁷⁸ Na sasa tunafahamu ya kwamba Uzao wa Ibrahimu haukuwa uzao halisi wa kujuana kimwili kupitia kwa Sara, ambao ulikuwa ni Isaka, ambao ulifanya taifa, bali ule uzao wa Kifalme ulikuwa kwa ile ahadi, ambao ulikuwa ni Yesu Kristo. Na kupitia kwa Uzao huo, Yeye alileta Uzao wa kifalme. Loo, jamani! Sasa sisi ni ukuhani wa kifalme, taifa la kifalme, taifa takatifu, tukitoa sifa kwa Mungu, dhabihu ya midomo yetu tukilitukuza Jina Lake. Mungu alithibitisha Neno Lake, alimmwaga Roho Mtakatifu juu yetu.

¹⁷⁹ Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika siku ile atakapokuwa akifunuliwa Mwana wa Adamu.” Sasa mliona? Kutoka Mwana wa Mungu, kabla tu hajafanyika Mwana wa Daudi, Yeye hujifunua tena kama Mwana wa Adamu. Je! mliyaona hayo Maandiko?

¹⁸⁰ Kwa kuwa, Yeye daima huwajulisha, Yeye hatendi lolote pasipokuwajulisha watumishi Wake hao manabii. Hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ndiyo iliyokuwa ahadi Yake. Unaona? Yeye hatendi neno lolote... Mungu hawezi kusema uongo. Yeye daima hulifunua, kwanza, kabla hajalitekeleza.

¹⁸¹ Angalia hali ya mambo tuliyo nayo leo. Angalia mahali tulipo. Kila mmoja wenu atakiri kwamba tuko katika Sodoma ya kisasa. Mnajua nchi hii itajuta. Hawana matumaini. Hakuna wokovu uliosalia kwa ajili ya taifa hili wala taifa lingine lolote. Tumevuka hayo sasa. Nabii zilizotabiriwa kuhusu jambo hili, zimetimia. Mungu anaokota masazo, akimwokota huyo kondoo mdogo popote alipo. Ataingia, moja ya siku hizi. Tuko katika wakati wa mwisho. Angalia, mahali tulipo.

¹⁸² Ninawauliza, kama tu ndugu ama dada, uweke msingi wa imani zaidi kwa muda kidogo tu kabla hatujawaombea watu hawa. Nami ninajua haitubidi kuondoka wakati wowote. Lakini ni—ni—ninataka kuanzisha mstari wa maombi, ndipo ninyi ambao itawabidi kuondoka mtaweza kuondoka basi. Unaona? Ninyi mnaotaka kubaki kwenye mstari wa maombi mnaweza kubaki. Lakini hebu mniruhusu tu mimi, kama ndugu, niwaonyeshe tu jambo fulani kwa muda kidogo.

¹⁸³ Mwangelie Yesu, katika Luka 17:30, unaona, wakati alipokuwa akisema pale kuhusu wakati wa mwisho, jinsi ambavyo wangekuwa kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu. Kisha akasema, “Na kama, kadhalika, katika siku za Sodoma,”

kasema, “wakati Mwana wa Adamu atakapokuwa akifunuliwa.” Mwana wa Adamu tena, sio Mwana wa Mungu. “Mwana wa Adamu,” unaona, hiyo inaingiza Malaki 4 tena, inaitimiza moja kwa moja. Nabii hizi zingine zote zikiingia moja kwa moja, jinsi ambavyo inapaswa kutimizwa. Yeye anathibitisha Neno Lake kuwa hivyo. Hiyo ni kweli.

¹⁸⁴ Basi angalia, kwa kufanya hivyo, jinsi atakavyoimwaga Roho Yake juu ya wote wenye mwili, na kile kitakachotukia, jinsi ambavyo kurudishwa kutakavyorudi. “Na wana wenu na binti zenu watatabiri. Juu ya watumishi wangu wanaume na wanawake nitaimwaga Roho Yangu. Nami nitaonyesha ishara katika Mbingu juu.”

¹⁸⁵ Nina picha hapa, ya Ndugu Lee Vayle hapa. Ningependa kuwaonyesha yale hasa yaliyotukia huko mlimani, hivi majuzi, wakati watoto wote wa shule walipotoka nje, kabla tu ya somo hili kubwa la kule kufunguliwa, hiyo Mihuri Saba. Wakati watoto wa shule walipotoka nje, wakati nilipokuwa huko juu nikiimba, huu hapa Moto katika umbo la faneli kabisa ukishuka, kisha ukapanda juu na kulipuka, kisha ukazungukazunguka na kushuka chini tena. Hivyo ndivyo alivyosema niende nikawaambie watu. Sisi...Hilo hapo, ambapo shule za Tucson...na pale ambapo ulipanda juu hewani.

¹⁸⁶ Na sayansi ilipiga picha, na kadhalika, na kuuliza maswali juu Yake. Walisema, “Uko wapi? Ni kitu gani kilichotendeka?” Hawaelewi ni kitu gani, unaona. Loo, halitendwi faraghani, ni dhamira tu iliyotiwa giza. Halijawahi...Yesu, wakati alipokuwa hapa, kulikuwa na mamilioni ya watu ambao kamwe hawakujua Yeye alikuwa duniani. Naam. Kutakuwa na mamilioni leo ambao hawatafahamu, makumi ya milioni wao.

¹⁸⁷ Bali kutakuwa, kwa wale Ambao limetumwa kwao, watafahamu. “Wenye hekima watamjua Mungu wao katika siku hiyo, na watafanya mambo makuu.” Tunatambua jambo hilo, saa ambayo tunaishi sasa.

¹⁸⁸ Angalia Sodoma sasa, angalia yale yaliyotendeka. Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.” Kulikuwa na kundi la watu waliokuwa wakimtaamia mwana aliyeahidiwa. Tunaamini jambo hilo. Hilo lilikuwa ni Ibrahimu na kundi lake. Kulikuwa na kundi vuguvugu, Lutu, aliyerudi nyuma nusu, hata hivyo ni mwamini; huko Sodoma. Makundi matatu ya watu.

¹⁸⁹ Daima kuna makundi hayo matatu. Watu wa Hamu, Shemu, Yafethi. Pia, waamini, wanaojifanya waamini, na wasioamini. Wako kila mahali, na sisi—sisi tunawakuta katika kila kundi. Na, kila mahali, unawapata. Na makundi hayo yangali yako hapa. Unapaswa kugawanya hilo. Unaweza kulipitishia moja

kwa moja kote katika Maandiko, linajiunganisha moja kwa moja vizuri.

¹⁹⁰ Sikilizeni jambo hili. Angalia mahali tunapoketi, mahali pake na kinabii, usiku wa leo. Sasa, kila mmoja wetu anajua ya kwamba ulimwengu uko katika hali ya Sodoma.

¹⁹¹ Tunajua nabii zote za Israeli, wako katika nchi yao. Kama ukitaka kujua kitaifa mahali tunaposimama, angalia Israeli, mahali ilipo.

¹⁹² Ukitaka kujua kanisa lina hali gani, angali jinsi wanawake wanavyoenenda. Mwanamke ni kanisa. Ukimwona, ni mzinzi, hana adabu; chungu, angalia mahali kanisa lilipo. Liangalie tu, unaona, unaona, waangalie tu wanawake. Unaona ambapo, jinsi wanawake wenu wanavyojivunja heshima na walivyochafuka sana, hivyo ndivyo kanisa lenu lilivyo, unaona, mfano.

¹⁹³ Angalia mahali Israeli ilipo, unaona mfano wa wakati mahali tulipo sisi. Unaona, angalia tu hizo ishara na maajabu. Kama wewe—kama wewe, ama kama macho yako yamefumbuliwa, angalia mahali tulipo sisi.

¹⁹⁴ Sasa angalia nafasi yetu mahali ambapo tupo, ulimwengu katika hali ya Sodoma. Sasa angalia, “kama hali ilivyokuwa.” Sasa angalia, kulikuwa na mtu fulani, katika siku ile, aliyekuwa akitarajia kuja kwa mwana aliyeahidiwa. Ibrahimu na Sara, walikuwa wakimtazamia mwana aliyeahidiwa katika kundi la Ibrahimu. Hawakuwa Sodoma. Lakini kwenye wakati huo tu, sura ya mwisho ya tukio hilo, kabla tu ya yule mwana aliyeahidiwa kuja, kulikuwa na watu watatu walioshuka kutoka Mbinguni, Malaika... Malaika wawili na Mungu. Nao walishuka wakaja na kuzungumza na Ibrahimu, chini ya mwaloni. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.] Na wawili wao walishuka wakaenda Sodoma na kupiga makelele dhidi ya dhambi ya jiji hilo. Na ilikuwa ni kabla tu ya kule kuteketezwa kwa ulimwengu wa Mataifa, wakati huo. Sodoma yote iliagamizwa papo hapo. Ni wachache tu waliovutwa wakatolewa, Lutu na binti zake wawili. Mkewe hata hakufaulu; aliangalia nyuma. Jinsi ambavyo ningetaka kuwa na wakati wa kuwaonyesha jambo hilo sasa hivi, mahali ambapo kanisa hilo linasimama mahali hapo. Ninataka muone jambo hilo sasa.

¹⁹⁵ Ndipo mtu mmoja akabaki nyuma, ambaye alizungumza na Ibrahimu, naye akamfanyia Ibrahimu ishara. Na, angalia, Ibrahimu alikuwa amemwona Mungu katika ishara nyingi kuu. Tunaamini jambo hilo, sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kabla tu ya kuja kwa yule mwana. Lakini kabla mwana huyo hajadhihirishwa, kulikuwa na ishara aliyopewa.

¹⁹⁶ Kwa sababu, Mwana, yule Mwana wa kweli, aliyekuwa awe ni Mwana wa Mungu, kupitia imani ya Ibrahimu, unaona,

alikuwa ni Yesu. Sisi tukiwa ni Uzao wa Ibrahimu, tukiwa tumekufa katika Kristo, sisi ni uzao wa Ibrahimu.

¹⁹⁷ Angalia sasa kabla tu jambo hilo halijatukia, mwana huyu aliyekuwa aje. Sasa, Huyu aliyekaa na kuzungumza na Ibrahimu, alikuwa amegeuza mgongo wake kuelekea kwenye hema, naye alisema, "Ibrahimu." Sasa, siku moja tu kabla ya jambo hilo, yeye alikuwa Abram. Sasa Yeye alisema, "Ibrahimu, yu wapi mkeo, Sara?" si Sarai, S-a-r-a-i. S-a-r-a, binti mfalme. "Yu wapi mkeo, Sara?"

Akasema, "Yumo hemani nyuma Yako."

¹⁹⁸ Akasema, "Nitakuzuru, unaona, kulingana na ahadi Yangu niliyokupa." Kwa maneno mengine, "Wakati wa maisha, Sara ataanza wakati wake wa kawaida wa maisha tena."

¹⁹⁹ Na Sara, akiwa mzee, umri wa miaka mia moja sasa, hemani, alicheka kisirisiri. Unaona, alitabasamu nafsini mwake, akasema, "Mtu huyo angeweza kusema kweli? Unaona, mimi nikiwa mwanamke mzee, bwana wangu Ibrahimu huko nje, pia ni mzee, uhusiano wa mume na mke ulikuwa umeachwa kwa muda wa miaka mingi." Kasema, "Ninawezaje tena kuwa na raha tena na bwana wangu? Yeye akiwa mzee, nami ni mzee, nimepita umri wa kuzaa, vena za maziwa zimekufa, kila... 'Yeye amekoma uzazi.' Tungeweza kamwe kupata raha tena?"

²⁰⁰ Naye Mtu huyo, akiwa ameelekeza mgongo Wake kwenye hema, alisema, "Kwa nini Sara amecheka, akisema, 'Mambo haya yanawezekanaje?'" Hicho kilikuwa ni nini? Utambuzi, jambo la kinabii! Unaona? Unaona? Hicho ndicho alichooa.

²⁰¹ Sasa Yeye alisema, "Hilo litarudi tena, na Mwana wa Adamu," ambaye alikuwa huyo, huyo alikuwa ni Mwana wa Adamu kabisa pale. Vema, yeye alimwita Elohimu, "Bwana Mungu." Elohimu, mtu yeyote anajua hiyo ni kweli, Elohimu ni Bwana Mungu. "Hapo mwanzo Elohimu aliumba mbingu na nchi," Yeye ajitoshelezaye kwa yote. Mwana wa Adamu aliyefanyika mwili, Huyo hapo alikuwa amesimama pale katika mwili wakati ule, kama theofani, amesimama pale akitambua yale Sara aliyokuwa akisema katika hema nyuma Yake. Yeye aliahidi. Angalia. Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu umeahidiwa kuona jambo lile lile.

²⁰² Lakini mwangalie Lutu, yeye alikuwa na ujumbe kule chini, pia, wawili wao walishuka kwenda kule. Mmoja wao alishuka kwenda kule, na mwingine akaambatana naye, nao walihubiri na wakawaita watu waikimbie hasira ijayo.

²⁰³ Hali ya mambo ilivyo sasa, ulimwengu haujawahi kuwa katika hali ile, tangu siku hiyo ambayo Yesu alitoa ahadi, mpaka sasa hivi kabisa. Ninataka kumwuliza mwanahistoria yeyote ambaye anaweza kuwa yumo jengoni, ama kama ukisikia hata kwenye kanda hii, na kusikia jambo hili wakati wowote, tafadhali uniandikie. Nimesoma historia sasa kwa muda wa

miaka thelathini, historia ya Biblia, wala hapajakuwapo na mtu ambaye nimepata kumwona katika historia yote ya kanisa, kupitia katika zile nyakati saba za kanisa. Ambapo sasa tuko katika Laodikia, na tunajua hivyo.

²⁰⁴ Kamwe hapajakuwa na mjumbe, ambaye alipata kwenda kwenye kanisa lote, ambapo jina lake linaishia na h-a-m, mpaka sasa. G-r-a-h-a-m, Billy Graham. Kumekuwa na akina Moody, Finney, Sankey, Knox, Luther, na kadhalika, bali kamwe sio h-a-m, “baba kwa mataifa.” Sasa kumbukeni, yeye ni G-r-a-h-a-m, herufi sita. Bali A-b-r-a-h-a-m ni herufi saba. Angalia, wako kule chini, Billy Graham, akienda katika—katika kila sehemu, na akiwaita kutoka Sodoma, “Tokeni, ikimbieni hasira ijayo.” Hakuna mtu ninayejua habari zake, aliye kwenye huduma, ambaye amemshikilia Mungu, katika Neno hilo la kuhesabiwa haki, kama Billy Graham anavyolishikilia. Anaweza hasa kulielezea. Yeye si mwanateolojia hodari. . .Nadhani yeye ni mwanateolojia, bali yeye si mwalimu hodari sana tu. Lakini Mungu yuko pamoja naye. Mtu huyo atasimama pale akiwa na kama somo la shule ya Jumapili, ateke usikivu wa watu hao sana. Yeye ni mtumishi wa Mungu kwa wakati huu. Kwa akina nani? Kanisa la kawaida, lililoko Sodoma.

²⁰⁵ Lakini kumbukeni, kulikuwa na kanisa moja la kiroho, ambalo halikuwa katika mpango huo wa kimadhehebu, kamwe. Kundi lililoitwa litoke, nao walipokea ujumbe, pia, na mjumbe. Na ilikuwa ni kitu gani? Kuyatambua mawazo yaliyokuwa moyoni. Mungu daima hulithibitisha Neno Lake.

²⁰⁶ Na tuombe. Baba mpenzi wa Mbinguni, wakati huu muhimu sana, ambapo maamuzi yanapaswa kutolewa, muda unasonga mbele, hatujui ni wakati gani Bwana wetu anaweza kuja. Nasi tunapooni nabii hizi ambazo zimetabiriwa na Yeye, kupitia kwa manabii Wako katika nyakati zilizopita, sasa zinafunuliwa. Ee Mungu, jinsi ninavyokushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hili, ya kwamba hata watu wenye afya nzuri, watu wanaojiweza katika—katika theolojia, ambao wanaweza kukabiliana na hila za ulimwengu na za wasioamini, na kwenye paneli hizi, na bila tashwishi yo yote wasimame pale wakiwa hodari na wenye ujasiri, wakijua mahali wanaposimama na kuthibitisha Neno hilo kuwa ni kweli, kwa Maandiko. Na halafu basi sisi ambao tunakungojea Kuja Kwako, Bwana, tukiamini mambo haya mengine ambayo yametabiriwa ambayo yangetukia, kusimama na kufurahia kukuona Wewe ukitembea moja kwa moja miongoni mwetu na ukifanya jambo lile lile ulilosema Wewe lingetimia, ukithibitisha Neno Lako kwamba ni kweli. Mungu wa milele, watoto Wako wagonjwa wameketi hapa.

²⁰⁷ Sijui kumesalia muda gani zaidi tulio nao tunaapaswa kufanya kazi. Jua la jioni linatua. Bali Wewe uliahidi, kwa nabii, “Itakuwa Nuru kwenye wakati wa jioni.” Na tunaona jua lile lile huchomoza mashariki, ndilo linalotua magharibi.

Ustaarabu umesafiri pamoja na jua na sasa tuko kwenye Pwani ya Magharibi, nayo Injili imesafiri pamoja na ustaarabu. Sasa, Baba, tunajua huu ndio mwisho wa Injili, mwisho wa wakati, mwisho wa kipindi cha wakati. Wakati unaishia katika Umilele. Lakini Wewe uliahidi ya kwamba Mwana atajitokeza, Mwana wa Adamu angefunuliwa. Katika siku ya mwisho, jambo hili lingetukia. Nuru za jioni zimekuja, Baba. Tunakushukuru kwa hilo. Na kwa unyenyekevu jinsi ilivyo, hata hivyo unafanya jambo hilo kwa urahisi sana, mara nyingi, hata linapita juu ya wanaodhaniwa kwamba wana akili nyingi sana, na unalifunulia watoto wachanga wanaoweza kujifunza.

208 Ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utalifanya litimie, usiku wa leo, ya kwamba maskini watoto Wako walio wagonjwa hapa wataona ahadi ya Mungu, na kila mmoja wao ataponywa, na watoke hapa, kesho, wakiwa na miili mipya yenye nguvu, na wapate afya tena. Tujalie, Bwana, ili kwamba waweze kuuchukua Ujumbe kutoka mtu mmoja hadi kwa mwingine, mpaka yule wa mwisho atakapoingia kwenye kundi, na ndipo milango itafungwa. Tusaidie, Mungu mpenzi. Ninakuomba, usiku wa leo, licha ya haya yote, kama utaninii tu mara moja zaidi, Baba, kwa ajili yangu.

209 Ili—ilionekana, hivi majuzi usiku, watu hawakuwa na habari nalo sana. Lakini, ninaomba, jalia litendeke tena usiku huu, Bwana. Maana, nimepitiliza wakati niliopangiwa kuzungumza, bali sijui ni kiasi gani cha wakati zaidi itatubidi kufanya jambo hili. Kwa hiyo, ninaomba, Baba, je! utanisikia? Na uyasikie maombi ya hawa wanaume na wanawake wacha Mungu wanaoketi hapa usiku wa leo, ambao wamejazwa na Roho Wako. Wao ni waamini, Bwana, unaweza tu kutenda kazi miongoni mwao. Nasi tunaninii... Ninaomba ya kwamba utathibitisha Neno Lako ulilosema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Jalia iwe hivyo tena, Yesu, kuthibitisha ya kwamba ni wewe yule jana, leo, na hata milele. Ninaomba jambo hilo kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Mwanawe, Yesu Kristo. Amina

210 Sasa, kwa muda kidogo tu, ninataka kujua ni watu wangapi hapa ndani walio na kadi za maombi. Ni—ninawataka mwinue mikono yenu, kila mmoja wenu aliye na kadi za maombi. Vema, ni kwa jumla, nakisia, ni karibu tu kila mahali.

211 Sijui ni watu wangapi hapa ndani wasio na kadi za maombi, na hata hivyo wewe ni mgonjwa, ungeinua mikono yako na kusema, “Sina kadi ya maombi, na hata hivyo mimi ni mgonjwa. Ni mhitaji.”

212 Ninataka kuwaomba muwe na kicho kwa muda kidogo. Sasa, ninapenda kuzungumza nanyi. Hiyo daima ndiyo shida yangu, ninazungumza kwa muda mrefu sana. Lakini kabla hamjakuja, ni—ningetumaini na kuamini ya kwamba Mungu

atathibitisha jambo hili na yale niliyosema kuwa ni Kweli, na mwache—mwache Yeye aone tu.

213 Sasa, ni wangapi walioketi huko nje walio wagonjwa, wanaojua ya kwamba sijui hata jambo moja kuwahusu, inueni mikono yenu. Hebu angalieni hilo. Vema.

214 Ninataka ninyi msio na kadi za maombi sasa. Kadi za maombi zitaitwa. Ninataka muombe.

215 Biblia ilisema ya kwamba, “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.” Yeye anasema, “Yeye ni Kuhani Mkuu aliyeketi huko akituombea tunapokiri.” Inatupasa kukiri kwanza, kabla hajaweza kuwa Kuhani Mkuu, maana yeye anaombea tu maungamo yetu. Hiyo ni kweli, enyi ndugu wahudumu? [Wahudumu wanasema, “Amina.”—Mh.] Unaona, Yeye hutuombea tu tunapokiri, yale tunayokiri kwamba ndivyo alivyo Yeye, yale Yeye aliyotufanyia. Sio yale Yeye atakayofanya. Yeye tayari amefanya. Inatupasa kukiri kwamba Yeye ameyafanya. “Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa mapigo Yake sisi tuliponywa.”

216 Sasa, Baba wa Mbinguni anajua. Na hivi nikiwaangalia, ni kuona ninamtambua rafiki yangu msiri kutoka Ohio, yeye na mkewe walioketi hapa, ni Bw. Dauch na mkewe. Nami ninaamini, anayeketi wa pili ama watatu kutoka kwao, ni yule Kasisi tena, Bw. Blair niliyemwona jana usiku. Kuna giza juu ya wasikilizaji, kwangu mimi, kwa sababu ya taa hizi hapa zinanipa ukungu kidogo, na si—siwaoni vizuri sana.

217 Lakini ninataka muombe. Na mweke moyoni mwenu jambo lile mnalohitaji, na mmuombe Kuhani wetu Mkuu, Ambaye anaweza kuchukuana nasi katika mambo ya udhaifu wetu.

218 Sasa, mimi pasipo kuwajua ninyi, na mngeweza kabisa kunigusa kila mahali, itakuwa ni kama kumgusa ndugu yako, mume wako, mchungaji wako, mtu fulani, halinge—halingefaa kitu. Lakini kama ukimgusa Yeye, na kama kweli sisi tuko sawa na Roho Wake, basi Yeye anaweza kutumia imani yako kumgusa Yeye, na kwa karama yangu kukujiibu.

219 Unaona, ningekuwa kimya tu kama hiki, hiki kilicho *hapa*, bila ya sauti inayozungumza kupitia kwake. Hapana budi iwepo... Hiki, hiki ni kimya pasipokuwapo na kitu hapa cha kuzungumza kupitia kwake. Na vivyo hivyo mtu yeyote, ni bubu, inapofikia kwenye mambo haya, isipokuwa Mungu azungumze kupitia kwao.

220 Sasa ninyi ombeni, na hebu na tuone kama mambo haya niliyosema ni kweli. Mungu, na alisaidie liwe hivyo. Sisemi kwamba Yeye atasaidia. Ninatumaini kwamba Yeye atasaidia. Ninatumaini kwamba atasaidia. Yeye kamwe hajanipungukia, kwa miaka yote, kote na kila mahali duniani, nikiwa na mataifa ya kila namna, na mamilioni ya watu. Yeye

kamwe hajanipungukia. Nami nina hakika, hakika tu kama ninavyoamini nimesimama hapa, hatanipungukia sasa.

221 Nitawaomba muwe tu na kicho na mwendelee kuketi chini, kwa dakika chache tu. Tataliruhusu kusanyiko kubwa liondoke kisha tuwaombee wagonjwa, punde si punde tu.

222 Lakini nawataka, ninyi waamini, kwamba endapo tu hamtanitegemea mimi, bali mtaamini. Semeni, “Ninaamini ya kwamba yale huyu mtu aliyosema ni Maandiko. Sijui kama tuko kwenye wakati ulioendelea sana kadiri yeye anavyotuambia. Lakini, kama ndivyo ilivyo, basi halina budi kutukia. Kama Maneno Yake ni Maneno ya Mungu, basi, maneno yake yatashindwa bali Maneno ya Mungu hayatashindwa.”

223 Mungu anawajibika kuunga mkono Neno Lake. Yeye atalithibitisha. Atalithibitisha. “Yeye aniaminiye Mimi.” Yeye alithibitisha ya kwamba hii ni siku ya mwisho. Alithibitisha jambo ambalo lingetukia. Alithibitisha ya kwamba jambo hili lilipaswa kutukia.

224 Na, kumbukeni, Ibrahimu na kundi lake kamwe hawakupokea ishara nyingine kutoka kwa Mungu, mpaka mwana aliyeahidiwa alipowasili. Ni wangapi wanaojua jambo hilo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hiyo ishara ya utambuzi! Nanyi Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, hebu niwasikie. . . Hebu niwaambie. BWANA ASEMA HIVI, Mnapokea ishara yenu ya mwisho. Hiyo ni kulingana na Maandiko na ufunuo wa Mungu ulio moyoni mwangu, ambao unasema ya kwamba huu ni Ukweli. Nami ninatumaini ya kwamba mtaliamini kwamba ni Kweli.

225 Sasa aminini. Kila mtu na aamini tu, aseme, “Bwana Yesu, nijalie nikuguse Wewe. Nina haja moyoni mwangu, na ninajua Ndugu Branham hajui kitu juu yangu. Hata simjui mtu huyu, hanijui mimi, bali Wewe unajua. Na endapo ameniambia Kweli, jambo hili litatukia.” Ninawaomba, msisogee sasa, kwa muda kidogo tu. Iweni kabisa. . .

226 Unaona, wewe ni roho. Nami ninachukua kila roho ndani hapa chini ya mamlaka yangu, katika Jina la Yesu Kristo, ili Neno Lake lipate kutimizwa.

227 Sasa iweni tu na kicho. Ombeni. Mwangalieni Yeye, msemi, “Bwana, ninaamini jambo hilo. Nisaidie kutokuamini kwangu.”

228 Hebu na tuanze. Inanibidi kuzingatia kwenye sehemu fulani ya jengo hili hapa, maana, unaona, mko wengi sana, na kila mmoja wenu, ni roho.

229 Siwezi. Unasema, “Na mimi je?” Nisingeweza kukwambia. Ni jambo la mamlaka iliyo kuu. Kazi zote za Mungu ni mamlaka kuu. Kutakuwa na watu wengi watakaoponywa wakipitia kwenye jukwaa hili, usiku wa leo, labda kutakuwa na wengi ambao hawataponywa. Yote yako kwenye mamlaka kuu ya

Mungu. Ni nani anayeweza kumwambia Yeye la kufanya? Hakuna yeyote. Yeye hutenda kazi kulingana na mapenzi Yake Mwenyewe, mpango Wake Mwenyewe.

²³⁰ Lakini ninyi aminini tu. Iweni wanyenyekevu. Msiwe na wasiwasi. Mwendeeni Mungu tu, na kusema, “Bwana Mungu, ninaamini hayo.” Unaona? “Nijalie niguse vazi Lako. Nina haja ya *hiki-na-hiki*. Ninajua ndugu huyu hanijui wala hajui haja yangu, bali alitwambia juu ya mambo haya uliyoyafanya, na anasema ya kwamba Wewe uko hapa yeye yule leo.”

²³¹ Hilo haliwaondoi ninyi ndugu hapa jukwaani, yeyote wenu. Ninawauliza tu, enyi ndugu zangu, kama wafanyakazi wenzetu wa—wa Injili ya Kristo. Ninazungumza nanyi kwa uaminifu tu kama nijuavyo, kama m—mtu anayekufa pamoja nanyi, unaona, anayeuga ulimwengu huu. Hatuna budi kuuaga. Nami sina budi kutoa hesabu kwenye Siku ya Hukumu, kwa ajili ya yale nisemayo. Ninajua jambo hilo, ninalijua sana. Nami ninawathamini ninyi watu, jinsi mlivyo, mkisimama hapa pamoja na mimi, mkinisaidia. Ninajaribu kuwasaidia, kufanya kila niwezalo, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

Ninaomba na kusihi.

²³² Hapa, ni wangapi waliopata kuona ile Nuru kwenye ile picha? Je! mmeona picha yake? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ile pale inaning’inia moja kwa moja *pale*. Hivi hamwezi kuona?

²³³ Iko juu ya bibi yule anayeketi pale akiwa na lesa yake. Anamwomba mpenzi wake mmoja. Hiyo ni kweli, bibi. [Huyo bibi anasema, “Hiyo ni kweli, Ndugu Branham.”—Mh.] Huyo mpenzi... Je! uniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama samahani, mtumishi Wake? [“Hakika ninaamini.”] Unaamini jambo hilo? Vema. Sasa, kama Mungu anaweza kunifunulia shida yako ni nini, mbona, utakubali jambo hilo kuwa limetoka kwa Mungu, kama tu yule mwanamke aliyegusa vazi Lake? Sasa, unajua wewe uko—uko futi ishirini ama thelathini kutoka kwangu, ama zaidi, hukunigusa mimi hata kidogo. Bali umegusa kitu Fulani, ambacho unajua unawasiliana na kitu Fulani, Mtu fulani. Jambo ni kwamba, ni kwa ajili ya mwanamke fulani, ambaye ni binti yako. Hiyo ni kweli. Je! unaamini ya kwamba ataponywa? Yeye ni mtumwa wa madawa ya kulevya. [“Hiyo ni kweli.”] Hiyo ni kweli kabisa. [“Hiyo ni kweli, ndugu.”] Ninamwona akiogelea, amelewa. Unaona? Sasa, lesa uliyo nayo mkononi mwako, iweke juu yake, wala usitie shaka. Ninaamini ya kwamba Mungu atamkomboa. Je! utaamini jambo hilo pamoja na mimi? Amina. [“Loo! Asante, Yesu!”]

²³⁴ Sasa, simjui mwanamke huyo, bali Mungu anamjua. Unaamini sasa kwa moyo wako wote?

²³⁵ Mwanamume yule anayeketi pale amevaa shati lenye milia, ana ngiri, unaamini ya kwamba Mungu angekuponya na

kukufanya mzima? Je! unaamini ya kwamba atafanya jambo hilo? Sijapata kumwona mtu huyo maishani mwangu. Je! bwana, una kadi ya maombi? [Mtu huyo anasema, “La, sina.”—Mh.] Ati huna? Huhitaji moja.

“Kama unaweza kuamini!”

²³⁶ Huyu hapa mwanamke ameketi akijaribu kuangalia juu ya mwanamke huyu anayeketi papa hapa. Hatufahamiani. Lakini yeye ana wasiwasi kweli kweli. Mimi simjui. Sijapata kumwona, maishani mwangu. Lakini Mungu anamjua, naye anatambua sasa hivi ya kwamba yeye anawasiliana na kitu Fulani. Umekuwa ukiomba pale kwa sababu fulani. Sababu ya kufanya hivyo ni kwamba, huwezi kudumu zaidi ya usiku wa leo. Huna budi kuondoka mkutanoni. Unajiandaa kwenda nyumbani kwako, kesho. Hutokei hapa, wala hutoki California. Unaelekea mashariki kutoka mahali hapa. Unaruka kwa ndege. Unajiandaa, unaenda kwa ndege. Unatokea Oklahoma. Naam. Hiyo ni kweli.

²³⁷ Wewe pia uko katika hali ya kufa. Umekuja hapa kuombewa. Huna kadi ya maombi. Lakini unaamini kwamba utaponywa, kama tu ungeweza kufika hapa. Hiyo ni kweli. Pia, ugonjwa wako ni kansa. Kansa hiyo iko kwenye mfupa. Unaamini utaponywa sasa? Unaamini umengusa Yeye, dada yangu? Labda Mungu ataniambia kwamba wewe ni nani, ndipo je! hilo lingekusaidia? Kama ndivyo, inua mkono wako kama unaamini jambo hilo, ya kwamba (Mungu) lingekusaidia. Vema, Bibi Steel, unaweza kurudi Oklahoma.

Simjui bibi huyo. Sijapata kumwona.

²³⁸ Huyu hapa bibi anayeketi papa hapa nyuma yake. Anaugua uvimbe wa veni. Na pia ana mwana ambaye ni mlevi sugu, naye anamwombea. Kama ataamini, anaweza kuponywa. Bibi Mason, je! utaamini kwa moyo wako wote na uamini ya kwamba Yesu Kristo atakupapa uponyaji? Je! unaamini?

²³⁹ Vema, basi weka mkono wako juu ya bibi huyo anayeketi karibu nawe pale, yeye anamwombea mume wake ambaye hajaokoka. Mungu atamjalia uponyaji.

Na tuombe.

²⁴⁰ Mungu mpenzi, ninaomba ya kwamba utampa baraka hiyo. Mpe mwanamke huyo shauku ya moyo wake, Bwana. Imani yake iko karibu sana na Wewe, imekugusa. Nami ninaomba, Baba, ya kwamba utasaidia, katika Jina la Yesu. Amina.

²⁴¹ Sasa amini kwa moyo wako wote, ya kwamba unaupokea. Je! utafanya jambo hilo? Vema. Mungu akubariki.

²⁴² Je! unaamini mume wako ataokolewa, bibi? Je! unaamini kwa moyo wako wote? Inua mkono wako, kwamba unaamini.

²⁴³ Inaonekana kuwapo, mbele yangu, yupo mwanamke ambaye ni mzito sana. Yule pale ameketi. Je! unaniamini kwamba mimi

ni mtumishi wa Mungu? Unaniamini kwamba mimi ni mtumishi wa Mungu? Unaamini? Vema. Sikujui. Shida uliyo nayo, ni tezi. Una uzito mkubwa kupita kiasi. Umekuwa kwa daktari, alisema asingeweza kufanya jambo lolote juu yake, bali huyo alikuwa ni daktari wa duniani. Unaona? Ninii yako. . . Ulikuwa tu na huzuni nyingi sana. Ulimpoteza mume wako. Hutoki hapa. Kusema kweli umetoka Arkansas. Unatafuta kazi, pia, wala huwezi kupata kazi. Ulikuwa unahofu kwamba, jambo fulani, hutaitwa. Lakini imani yako sasa imengusa Mungu. Dada yangu, nenda, amini. Mungu na akupe kazi, akupe shauku ya moyo wako.

244 Mungu huthibitisha Neno Lake kuwa ni kweli. Je! mnaamini jambo hilo kwamba ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa nataka tu muombe pamoja nami tena.

245 Baba, Mungu, Wewe ni Mungu yeye yule aliyethibitisha. Wakati uliposema, "Msichana huyo hajafa, amelala," kisha ilikubidi kulithibitisha jambo hilo. Sasa, Wewe uliahidi, ya kwamba kabla tu ya kuja kwa wakati wa mwisho, ya kwamba Mwana wa Adamu angejifunua kwa jinsi ile ile aliyojifunua huko Sodoma. Uliahidi jambo hilo, Bwana. Sasa umekuwa duniani katika mfano wa Roho Mtakatifu, na ukaingia miongoni mwetu, usiku wa leo, sisi watu tunaamini, nawe umethibitisha jambo hilo. Umethibitisha Neno Lako kama ulivyofanya siku ile. Bwana, hatuhitaji thibitisho lingine. Wewe uko miongoni mwetu. Tunakupenda. Pia tunatambua ya kwamba hii ndiyo ishara ya mwisho kabla tu ya Kuja Kwako, kulingana na Maandiko. Na vivuli vyote na mifano havikosei kamwe. Havina budi kuwa halisi.

246 Kwa hiyo tunaomba, Baba, wakati watoto Wako wanapokuja sasa kuombewa, ya kwamba kila mmoja ataponywa. Jalia pasiwe na mgonjwa aliyesalia miongoni mwetu, mwishoni mwa ibada hii ya uponyaji. Ee Mungu mpendwa, Utajalia upako Wako uwe juu ya watu Wako kwa neema sasa hivi, kusudi kila mmoja wao apate kuponywa?

247 Na kama kukiwa na wengine hapa, ambao si watoto Wako bado, na juu ya msingi wa mambo haya, ya kwamba. . . Wamelisikia Neno, na kuona mambo yakitendeka, yakithibitishwa wazi wazi kabisa, na kwamba Wewe ni Nani na kile Ulichu, ya kwamba Uko hapa.

248 Na, Bwana, je! Wewe—Je! Wewe ungeweza kubariki uongo? Mbona, bila shaka huwezi, Bwana. Lakini uliahidi kulibariki neno Lako, wala halitarudi bure. Litatimiza kile lililokusudiwa. Na sasa umefanya jambo hilo mbele zetu, usiku wa leo, pasipo shaka yoyote.

249 Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, je! kuna watu hapa ambao hawajaamini hapo awali, kwamba ungetaka kuinua tu mkono wako? Huku kichwa chako kimeinamishwa, hebu inua

tu mkono wako. Na usimame kwa miguu yako, na useme, “Sasa ninaamini, kwa moyo wangu wote. Nami ninataka kumkubali Yesu Kristo, sasa hivi.” Je! mngefanya jambo hilo, watu wowote, watu wowote waliopo hapa, ambao bado hawajampokea Kristo, nao wangetaka kufanya jambo hilo wakati huu? Sitawaambia... Nendeni kwenye kanisa mnalotaka. Lakini ninawaomba kumpokea Yesu Kristo wakati mki-... Labda hamtakuwa karibu zaidi Naye mpaka mtakapomwona uso kwa uso wakati atakapokuja katika mwili Wake unaoonekana kutoka Mbinguni. Je! sasa mtampokea kama tayari hamjafanya jambo hilo?

²⁵⁰ Juu ya msingi wa kutomwona mtu yeyote hapa amesimama, ninaamini basi ninyi nyote kuwa mna akili timamu, watu wenye hekima, na mnatambua yale mnayofanya. Kama mnaketi hapo chini ya hili, kumbuka, “Mkinionea haya mbele ya wanadamu, nitawaonea haya mbele ya Baba Yangu.” Kulikuwa na mtu aliyekuwa akisimama, labda, naam, katika wasikilizaji, huko nyuma.

²⁵¹ Mungu mpenzi, hao wanaweza, sioni, ambao wamesimama, wanataka kukukubali. Wanatambua, Bwana, ya kwamba jambo hili halijatendwa mpaka wakati huu, na sasa unalihakikisha na kulithibitisha kwamba ni kweli. Ninaomba, Baba, ya kwamba katika mioyo yao, iliyochochewa kiajabu wakati huu... Tunajuaje hata hivyo kwamba huyu ndiye mtu wa mwisho kuingia? Huu huenda ukawa ndio mwisho wa Los Angeles. Hii huenda ikawa ndiyo nafsi ya mwisho kuzaliwa katika Ufalme. Hatujui lini wakati huo utakapokuja. Na hapo utakapokuja, mlango utafungwa, ule Mwili utakamilishwa. Hautakuwa ni kioja cha mwili wala kioja cha Bibi-arusi. Utakuwa tu na kiasi fulani cha wafuasi ambao majina yao yaliwekwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ambao Yesu alikuja kuchukua, kama vile ilivyokuwa Adamu, alivyotoka moja kwa moja akaenda kumwoko mke wake. Naomba, Mungu, ya kwamba utawapokea sasa katika Ufalme Wako. Wamo mikononi Mwako. Washughulikie, Bwana, naomba katika Jina la Yesu. Amina.

²⁵² Mungu na ambariki kila mmoja wenu aliyesimama. Sikujua baadhi yenu mlikuwa mmesimama. Wengine walisimama huko nyuma, wengine huko katika roshani. Sasa ninataka mnifanyie jambo moja. Naomba mnielewe. Kutaneni na mhudumu fulani hapa na mzungumze nao, baada ya kanisa kutoka. Je! mtafanya hivyo? Msikose. Kama hujawahi kubatizwa katika ubatizo wa Kikristo, fanya hivyo, kisha uendelee kuinua mikono yako juu mpaka utakapompokea Roho Mtakatifu.

²⁵³ Sasa, na watu wengi wana kadi za maombi hapa. Tutawaomba wasimame, na waje hapa, na nafikiri wavuke upande huu. Ama itanibidi kuja... [Mtu fulani anasema, “La.”—Mh.] Sitaweza. [“Njoo kutoka upande huu hapa.”] Kutoka

upande *huu* hapa, mnaweza kutoka kupitia hapa, upande huu, watu walio na kadi za maombi.

²⁵⁴ Na sasa kama kuna mmoja wenu ambaye hana budi kuondoka, ni... nimechelewa. Samahani. Nitajaribu kufanya vizuri zaidi kesho usiku. Kwenye... ni saa nne na dakika kumi, kulingana na saa iliyoko ukutani. Asanteni sana kwa kuhudhuria kwenu usiku wa leo, na Mungu wa Mbingu na awabariki. Kama ungetaka kubaki na kuangalia mstari wa maombi, daima unakaribishwa. Lakini tutaanza kuwaombea wagonjwa sasa, nami sitaki kuwachelewesha isipokuwa iwe mnataka kukaa. Mmeruhusiwa kuondoka katika Jina la Bwana Yesu. Amani ya Mungu na iambatane nanyi na kuwabariki, na iwape raha miilini mwenu, usiku kucha, na awape afya njema kusudi muweze kurudi tena kesho usiku. Mungu awe pamoja nanyi sasa.

²⁵⁵ Na hebu wale walio na kadi za maombi wasimame kwa ajili ya maombi sasa, tunapowaombea watu toka kila mahali. Sasa tunataka mjue, sasa, ninyi mnaosimama mkiwa na kadi ya maombi, je! kuna shaka yoyote maishani mwenu? Kuna yoyote, samahani, dhambi yoyote maishani ambayo hujaitubia? Ikiwapo, hebu nikuombe jambo hili. Usije kwenye mstari wa maombi ukiwa na dhambi isiyotubiwa moyoni mwako. Maana, huna budi... Huu ni mkate wa watoto, unaona. Na endapo wewe si Mkristo, yasalimishe maisha yako kwa Kristo, katika mstari wa maombi, kisha uje. Ni kwa ajili ya mwaminio. Je! utafanya hivyo? Mkubali kwanza kama Mwokozi wako, kisha uje huku jukwaani, upate kuombewa.

²⁵⁶ Sasa nitamwombea kila mtu binafsi; si kuwapitia tu, kama namna fulani ya utaratibu. Tuko kanisani sasa. Nafikiri Dada Wyatt ametupa sababu ambayo tunaweza kukaa na kuomba. [Mtu fulani anasema, “Naam, usiku kucha, kadiri mtakavyo.”—Mh.] Tunaweza kukaa kirefu kadiri tutakavyo. Nami ninamshukuru Dada Wyatt na wafanya kazi hapa, kwa kuturuhusu kufanya hivyo. Mungu ambariki. Mume wake shujaa alisimama kwenye jukwaa hili, akawaombea wagonjwa, mpaka alipokufa, kadiri niuavyo mimi, askari halisi wa msalaba. Na sasa ninajaribu kuendelea kufanya jambo lile lile, kuwabariki watu hawa.

²⁵⁷ Na sasa ninaomba ya kwamba kila mmoja wenu atakayepitia hapa... Si lazima ukiri chochote unachotaka. Haikulazimu kusema shida yako ni nini. Njoo tu na uache nikuombe, na uamini.

²⁵⁸ Je! mnaamini ya kwamba Mungu amenituma kufanya jambo hili? Inua mkono wako. Mnakumbuka vile Malaika wa Bwana alivyosema? “Ukiwafanya watu wakuamini wewe, uwe mwaminifu unapomba, hakuna kitakachosimama

mbele ya maombi hayo.” Nanyi mnajua jambo hilo ni kweli. Limethibitishwa, tena na tena.

259 Sasa nitaomba ya kwamba Dada yetu Rose, akiweza, apige ule, *Amini Tu*, ama, *Ni Tabibu wa Karibu*, ama kitu fulani.

260 Ninataka kila mmoja wenu sasa muwe—muwe katika ushirika na mimi. Mtafanya hivyo, pia, ninyi watu msio kwenye mstari wa maombi, je! mtakuwa mkiwaomba watu hawa? Vema, waahidi jambo hilo, kwa kuinua mkono wako, “Nitakuwa nikiomba, unaona. Sote tutakuwa tukiomba.” Vema. Naam.

261 Ningetaka kwamba mninii, ikikubidi kuondoka, ondoka kimya sana sasa, ili kwamba wasiwasumbue wakati tukiomba.

262 Je! unaamini yatakwisha sasa, dada? [Huyo dada anasema, “Kwa moyo wangu wote.”—Mh.]

263 Mungu mpenzi, ninaweka mikono yangu juu ya dada, nikiyapa mateso ya mwili wake changamoto. Katika Jina la Yesu Kristo, na yamwache. Amina.

Akubariki, dada.

264 Unaamini kwa moyo wako wote? Dhambi zako zote zimetubiwa? Umetubu, kadiri ujuavyo wewe, uko tayari kupokea uponyaji wako?

265 Mungu mpenzi, ninaweka mikono yangu juu ya dada yangu, katika Jina la Mwanao, Yesu Kristo, na kuomba ya kwamba mateso haya ya mwili wake yatakwisha, katika Jina la Yesu. Amina.

266 Je! dhambi zote zimetubiwa, nawe uko tayari kwa ajili ya uponyaji wako? Unaamini, ndugu? [Huyo ndugu anasema, “Ninaamini kwa moyo wangu wote.”—Mh.]

267 Mungu mpenzi, ninaweka mikono yangu juu ya ndugu yangu, kwa kuwa tunajua ya kwamba Wewe upo hapa, Bwana. Ninaomba ya kwamba utamponya, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

268 Dhambi zote zimetubiwa? La, husikii. [Ndugu Branham anazungumza pole pole na kwa udhahiri kwa sababu ya uziwi wa huyo dada—Mh.] Unaamini ya kwamba utasikia? [Huyo dada anasema, “Ninaamini. Lakini nimekuwa kiziwi.”] Wewe amini.

Mwanamke huyu ni kiziwi sasa. Tuingie katika maombi hapa.

269 Mungu mpenzi, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu, na umwondolee uziwi huu. Yeye ameketi katika ulimwengu uliotengwa nje, ambapo hawezi kusikia. Ninaomba ya kwamba utampa uponyaji wake, kwa Jina la Yesu.

270 Nitawaomba watu waendeleo kuinamisha vichwa vyao, kwa muda kidogo. Ninataka kuona kilichompata. Sasa, tafadhalini, katika Jina ya Yesu Kristo, hebu mtu yeyote asiinue kichwa

chao wala macho yao. Sasa, haiwapasi kufanya hivyo mpaka nitakapowaambia.

²⁷¹ Unaweza kunisikia sasa? [Dada anasema, “Sio dhahiri.” Ndugu Branham anapiga makofi mara moja. “Ninaweza kusikia.”—Mh.] Unanisikia? [“Kidogo.”] Unaweza kusikia? Anaweza kusikia sasa. [Ndugu Branham anapiga makofi mara nyingine tena.] Unaona? Unasikia sauti hiyo?

²⁷² Sasa wewe amini kwa moyo wako wote. Utafanya hivyo? Nawe uamini, na Mungu atakufanya mzima kabisa. Yeye alisema. Niliomba tu na kuweka mikono yangu kwenye masikio yake, naye alisema angeweza kusikia kitu fulani. Vema, endelea tu sasa, ukiamini ya kwamba utasikia tena vizuri kabisa, nawe utasikia.

²⁷³ Je! dhambi zote zimetubiwa, dada? [Huyo dada anasema, “Naam.”—Mh.] Uko tayari kwa ajili ya uponyaji wako? [“Naam.”]

²⁷⁴ Mungu mpenzi, ninaweka mikono yangu juu ya dada yangu, nikijua ya kwamba ndani yetu hamna jambo jema, katika nafsi zetu. Ila tunajua ya kwamba sisi ni Wakristo, tuliozaliwa kwa Roho wa Mungu. Nasi tunaweka mikono yetu juu ya dada yetu na kuombea uponyaji wake, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁷⁵ Sasa je! unaamini utapona? [Huyo dada anasema, “Vizuri sana!”—Mh.] Vema, sasa u—umeponywa. [“Naam!”] Hiyo ndivyo njia ya kufanya jambo hilo. Hiyo ni kweli. Sawa.

²⁷⁶ Je! dhambi zote zimetubiwa? [Huyo dada anasema, “Naam, bwana.”—Mh.] Nawe uko tayari kwa ajili ya uponyaji wako? [“Naam.”] Unaamini, kwa kuwekea mikono, ya kwamba Mungu Ambaye anajua mioyo ya watu, atakuponya? [“Ninaamini.”]

²⁷⁷ Baba yetu wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu, tunapoweka mikono yetu juu yake na kuomba katika Jina la Yesu Kristo ya kwamba utamponya. Amina.

²⁷⁸ U hali gani? Bila shaka, unajua ninajua shida yako. [Dada anasema, “Naam.”—Mh.] Lakini sio kwamba ninajisemea tu; sababu, unajua, ita—itazidi kuendelea na kuendelea. [“Vema.”] Lakini kama utaninii. . . Je! dhambi zote zimetubiwa? [“Ndio, bwana.”] Na unaamini ya kwamba Mungu atakufanya mzima? [“Ndio, bwana.”] Je! unaamini ya kwamba yabisi kavu. . . Tayari nimeitaja.

²⁷⁹ Mungu mpenzi, ninaomba ya kwamba utamsaidia na kumfanya mzima. Mjalie, katika Jina la Yesu.

Hutakuwa kiwete. Nenda, amini kwa moyo wako wote.

²⁸⁰ Je! unaamini ya kwamba Mungu atakufanya mzima? [Huyo dada anasema, “Amina.”—Mh.] Dhambi zote zimetubiwa nawe uko tayari kwa ajili ya uponyaji wako? Unaamini mgongo wako utakuwa sawa?

281 Mpenzi Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya na kumpa afya. Katika Jina la Yesu Kristo, na iwe hivyo. Amina.

Mungu akubariki, dada. Nenda, ukiamini sasa.

282 Je! dhambi zote zimetubiwa, dada, uko tayari kwa ajili ya uponyaji wako?

283 Mungu mpenzi, dhambi zake, yeye anasema, zimetubiwa. Ninaweka mikono yangu juu ya mwanamke huyu, katika Jina la Yesu Kristo, naomba apate kuponywa. Amina.

284 Je! dhambi zote zimetubiwa? Huna budi kuwa sahihi, wewe ni mgonjwa sana, unajua jambo hilo. Unajua ya kwamba ninajua shida yako ni nini. Na je! unaamini ya kwamba Mungu atakufanya mzima, auponye moyo wako na kukufanya mzima kabisa?

285 Mungu mpenzi, ninaomba kwamba katika Jina la Yesu Kristo, ya kwamba utamponya na kumfanya mzima. Jalia huu umwondoke, Baba, katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu akubariki sasa. Usitilie shaka. Nenda, ukiamini.

286 Dhambi zote zimetubiwa? Uko tayari kwa ajili ya uponyaji?

287 Baba mpenzi wa Mbinguni, ninaweka mikono yangu juu ya dada yetu. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

Usitilie shaka, nenda, ukiamini.

288 Je! dhambi zote zimetubiwa? Uko tayari kwa ajili ya uponyaji?

289 Baba mpenzi wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya ndugu yetu, utampa afya. Mjalie, Baba. Ninaweka mikono yangu juu yake, kwa ajili ya kusudi hili, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki. Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote.

290 Je! unaamini sasa, dada? Je! dhambi zote zimetubiwa na uko tayari kwa ajili ya uponyaji?

291 Mungu mpenzi, ninaweka mikono yangu juu ya dada, katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

292 Sasa mara nyingi tu namna hiyo, mguso tu, kama Yesu alivyosema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa." Nimeanza kuona, katika mikutano, ya kwamba inaleta asilimia hamsini ya matokeo mazuri kuliko inavyofanya wakati ukiwaita watu kwenye mstari, unafanya utambuzi, maana unawafikia wachache tu. Na, kwa njia hii, kuna wengi zaidi wanaoponywa.

293 Je! umetubu dhambi zako zote za kutokuamini na kila kitu? Je! unaamini sasa ya kwamba utaponywa? [Huyo dada anasema, "Naam, na kukombolewa."—Mh.]

294 Mungu mpenzi, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu wakati nikishika mikono yake na kuomba katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

Mungu akubariki, dada.

295 Je! unaamini sasa? [Huyo dada anasema, “Ndio.”—Mh.] Dhambi zote zimetubiwa? [“Ndio.”]

296 Mungu mpenzi, ninaweka mikono yangu juu ya dada yetu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

Mungu akubariki, dada.

Linaonekana kama ni jambo dogo sana, bali Mungu ndiye ameliahidi.

297 Je! dhambi zimetubiwa?

298 Mungu mpendwa, ninaomba ya kwamba utamponya huyu dada yetu. Ninapoweka mikono juu yake katika Jina la Yesu Kristo, jalia aende na awe mzima. Amina.

299 Je! Dhambi zimetubiwa?

300 Mungu mpenzi, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu, ninapomwekea mikono, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

301 Sasa unapokuja na mitambo, na iguse zile nguvu tendaji, itatenda kazi.

302 Je! dhambi zimetubiwa? [Huyo dada basi anajibu—Mh.] Uko tayari.

303 Mungu mpenzi, ninaomba ya kwamba utamponya na kumfanya mzima, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki, dada.

304 Dhambi zote zimetubiwa? [Huyo dada anasema, “Kila kitu.”—Mh.]

305 Mungu mpenzi, wakati mwanamke huyu ananiangalia machoni, ninaamini jambo hilo. Ninaomba ya kwamba utamponya, katika Jina la Yesu.

306 Wewe unamleta tu, sivyo, dada? Unamleta tu? Vema. [Huyo dada anasema, “Yeye ni kipofu, pia.”—Mh.] Unaamini, dada, ya kwamba Mungu atakuponya? [Huyo dada kipofu anasema, “Ninaamini Mungu angeweza kunipa kuona tena.”] Mungu akubariki.

307 Baba wa Mbinguni, Wewe daima unawarehemu vipofu, na kwa wahitaji. Sasa wameona yale umefanya usiku wa leo. Kwa hiyo tunaamini, Bwana, ishara hii kuu ya mwisho ikitenda kazi miongoni mwetu sasa. Ninaomba kuona kwa mwanamke huyu kipofu kumrudie, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

308 [Yeye aliyekuwa kipofu, anasema, “Asante, Yesu.”—Mh.] Sasa, tupe taarifa ya jambo hili sasa. Toa taarifa yake. [“Nitaitoa!”]

309 [Yeye aliyemleta huyo dada kipofu, anaomba maombi—Mh.] Loo, naam, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? [“Haleluya!”]

310 Baba yetu Mpenzi wa Mbinguni ninaweka mikono yangu juu ya dada yetu na kuomba ya kwamba umponye, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

311 Mungu akubariki, dada. Hebu na tusikie jinsi—jinsi unavyoendelea.

312 Je! Unaamini, dada? [Huyo dada anasema, “Naam, ninaamini.”—Mh.]

313 Ee Baba mpenzi wa Mbinguni, ninamwomba dada yetu, nikitumaini ya kwamba utamponya sasa hivi. Ninaweka mikono yangu juu yake, katika Jina la Yesu Kristo.

Sasa amini. Hiyo ni kweli. Nenda tu, ukiamini.

314 Je! unaamini, ndugu? [Huyo ndugu anasema, “Naam.”—Mh.] Dhambi zote zimetubiwa?

315 Mungu mpenzi, ninaomba ya kwamba utamponya ndugu yetu na kumfanya mzima, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

316 Unaamini, dada?

317 Ee Mungu, ninaomba ya kwamba, katika Jina la Yesu Kristo, kwa unyenyekevu, katika utamu na upole wa wakati huu, jalia Roho Mtakatifu amponye mwanamke huyu. [Dada anasema, “Pia ninaomba, umwombee mwanangu. Sijamwona kwa muda wa miaka ishirini.”—Mh.] Ninaomba ya kwamba Mungu atamtuma mwanao kwako, dada, mpendwa. Mungu akubariki.

318 Baba mpenzi, ninamwomba dada yetu hapa. Katika utamu wa Roho Mtakatifu, jalia aje sasa na kumponya dada yetu, katika Jina la Yesu. Amina.

Akubariki, dada.

319 Mungu mpenzi, ninamwomba ndugu yangu, anaposimama hapa nami ninaweka mikono juu yake, na kuomba kwa ajili ya kuponywa kwake, katika Jina la Yesu.

320 Akubariki, ndugu yangu. [Huyo ndugu anasema, “Mungu akubariki.”] Vema.

Mvulana mdogo?

321 Mungu mpenzi, ninaweka mikono juu ya mtoto huyu, ninambariki katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake.

322 Unaamini sasa, dada? [Huyo dada anasema, “Naam.”—Mh.] Wewe pia unataka kuombewa?

323 Mungu mpenzi, ninamwomba, ninapoweka mikono juu yake. Sasa, hili ni agizo Lako, hivyo ndivyo ulivyosema tufanye. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono

yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Ulisema hivyo, Bwana. Amina.

Sasa, Yeye alisema hivyo, sivyo? Inapaswa kuwa hivyo, dada.

³²⁴ Mungu mpenzi, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu na kumfanya mzima, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Mungu akubariki, dada.

³²⁵ Je! umekuja ukiamini, dada?

³²⁶ Mungu mpenzi wa Mbinguni, ninaomba baraka Zako juu ya dada yetu, nikitii tu yale uliyosema tufanye. Ulisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa,” Wewe ulisema, “watapata afya.”

³²⁷ Hebu nisimame hapa kwa muda kidogo tu, kusema kuhusu jambo hili, kusudi tu niwaache watu wapumzike kidogo, kwa muda kidogo tu. Mkosoaji mmoja siku moja aliniambia, mimi, hivyo sivyo. Lakini, unaona, Yeye alisema, “Ishara hizi zitafuata.”

³²⁸ Mmesikia Ujumbe wangu juu ya *Lile Shtaka*, kumshtaki Yesu. Unaona, Yeye alimwambia Nuhu, “Itanyesha.” Haikunyesha hata kidogo kwa miaka mia moja na ishirini, bali ilinyesha hata hivyo. Alimwambia Ibrahimu angempata mwana kwa Sara. Ilikuwa ni miaka ishirini na mitano baadaye. Yeye kamwe hakusema ni lini. Alisema watampata huyo mwana. Miaka ishirini na mitano baadaye, ilitendeka. Unaona. Yeye hakusema ni lini.

³²⁹ Alisema, “Maombi ya imani yatawaokoa wagonjwa. Mungu atawafufua. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapona.” Je! hivyo ndivyo alivyosema? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye hakusema wataruka juu na kupona papo hapo. Alisema, “Watapata afya.” Unaona, hiyo ndiyo ahadi Yake. Hivyo ndivyo tunavyoamini.

³³⁰ Njoo, dada. Je! unaamini jambo hilo kwamba ni kweli? [Huyo dada anasema, “Naam, ninaamini.”—Mh.] Basi hakuna njia ya kukuzuia usiponywe.

³³¹ Ninaweka mikono yangu juu ya dada, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

³³² Je! unaamini, dada? [Huyo dada anasema, “Naam.”—Mh.] Dhambi zote zimetubiwa, nawe uko tayari?

³³³ Mungu mpendwa, ninaweka mikono yangu juu ya dada, kwa kutii amri Yako, na kuomba kuponywa kwake, katika Jina la Yesu. Amina.

³³⁴ Ninataka ninyi ambao mnaombewa, ninataka mniunge mkono. Ninawataka mtoe taarifa, kabla mikutano hii haijakwisha, kile kinachotukia; na muwaonyeshe wasikilizaji, hao watu wengine, waone ni jambo gani hasa linalotukia. Labda

kesho, kesho kutwa, ama wakati wowote ule, angalieni tu jambo litakalotukia.

335 Barua zangu zimeonyesha ya kwamba ni—ni tofauti sana na kuwaacha tu wajaribu, kujaribu imani zao wenyewe. Kwa sababu, Yesu alisema, “Wanaweka mikono juu yao. Wanaiweka mikono juu yao, watapata afya.” Sasa shika alilosema. Hakusema wangeruka juu na kukimbia huku na huko sakafuni. Wangeweza kufanya hivyo. Bali Yeye alisema, “Watapata afya.” Je! hivyo ndivyo alivyosema? Hivyo ndivyo alivyosema. Hivyo ndivyo ninavyoamini. Na Yeye yuko hapa sasa, Yeye aliyesema Neno Yuko hapa kulitimiza.

336 Unaamini, bwana? [Huyo Ndugu anasema, “Amina.”—Mh.]

337 Baba mpenzi wa Mbinguni, kwa kukiri imani yake na kuamini, ninaweka mikono yangu juu yake, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake.

338 Mungu mpenzi, ninaweka mikono juu ya mwanamke huyu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake. Vema.

339 Baba mpenzi, ninaweka mikono juu ya mwanamke huyu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake. Wewe ulisema, “Atapata afya.”

340 Uko tayari kwa ajili ya uponyaji, dada?

341 Mungu mpenzi, ninaweka mikono juu yake, katika Jina la Yesu Kristo, upate kumponya.

342 Vema, dada, mpenzi, kila kitu kiko tayari kwa ajili ya uponyaji? Je! imani yako sasa imetimia, unaamini utapona?

343 Na, Mungu, ninaweka mikono yangu juu yake, katika kutii agizo Lako, “Ulimwenguni kote, kwa kila kiumbe.” Ninaweka mikono juu yake, katika Jina la Yesu, kwa ajili ya uponyaji wake.

344 Mungu mpenzi, ninaweka mikono yangu juu ya ndugu yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake.

345 Mungu mpenzi, ninaweka mikono yangu juu ya dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wake.

346 [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]...akipitia kwenye marefu ya kanisa. Kamwe sikutaka kukuchosha. Utakuwa mzima kama utaamini jambo hilo sasa.

347 Mungu mpenzi, ninaomba ya kwamba utamponya dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

348 [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]...kunisaidia kuwaombea watu hawa.

349 Sasa tuna leso kadha hapa, na kadhalika, hapa ndani, za kuombewa. Nami ninataka muendeleo kuomba pamoja nami sasa, sasa, vifurushi hivi vidogo, sasa. Ninajua jambo hili linasikika la kigeni sana kwa watu kuomba kitu kidogo kama hiki. Lakini laiti ungalikuja uingie ofisini mwangu, siku moja, na kuangalia tu. Kama tungalikuwa tumeweka shuhuda

katika miaka hii yote, nafikiri usingaliweza kuzilundika juu ya jukwaa hili, ambao wameponywa kwa kutumiwa tu lesi hizi zilizooombewa namna hii, mamilioni yake, kote ulimwenguni. Sasa, unajua kwamba ni kitu gani—ni kitu gani?

³⁵⁰ Mtu fulani achukue lesi hiyo pale ya yule—yule nanii mdogo. . . Utajua lesi yako, sivyoyote, ndugu? Sawa.

³⁵¹ Nami nimewaona watoto wadogo, viwete, wakiponywa. Na unaona, jambo ni kwamba, ni suala la mahali hasa pa mawasiliano, kama Oral Roberts alivyozoea kusema. Ni mahali hasa pa mawasiliano. Tunaomba. Sasa, hatufanyi jambo hili sisi wenyewe, tunafanya jambo hili kwa sababu Biblia inatuagiza kufanya hivi. Sote tunajua hiyo ni kweli.

³⁵² Sasa, kuna watu wengi ambapo wanatia lesi mafuta, na kadhalika. Vema, sasa, tunafikiri hilo ni sawa, hakika, lakini kama tukinini tu. . . Biblia haikusema ya kwamba “walitia lesi mafuta.”

³⁵³ “Bali walichukua lesi kutoka katika mwili wa Paulo.” Sasa unaona kile nilichokuwa nikizungumzia? Sasa, kile walichoona, zile nguvu za kuhuisha zilizokuwa ndani ya Paulo, kwamba walijua yeye alikuwa ni mtumishi wa Mungu. Walijua ya kwamba Mungu alikuwa ndani yake. Walijua ya kwamba kila kitu alichogusa kilibarikiwa. Ni wangapi wanafahamu jambo hilo? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

³⁵⁴ Unajua, nafikiri Paulo alikuwa ni wa Kimaandiko kabisa katika yale aliyofanya. Hivi wewe unaonaje? Unataka nikwambie mahali alipopata wazo hilo la kufanya jambo hilo? [Mtu fulani anasema, “Kutoka kwa Elisha.”—Mh.] Kutoka kwa Elisha, sawa. Unaona, Eliya alisema, “Chukua fimbo hii na uende ukaiweke juu ya mtoto huyo mchanga.” Naye huyo nabii alituma hiyo fimbo kwa kuwa alijua ya kwamba kila alichogusa kilibarikiwa. Alijua nafasi yake. Yeye. . . kama angeweza tu kumfanya mwanamke huyo kuamini jambo lile lile.

³⁵⁵ Sasa unaona, sasa, Biblia hata kamwe haikusema, “Watawaombea wagonjwa.” Ilisema, “Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa.”

³⁵⁶ Sasa wazia tu, watu hao waliona, kwa mtume Petro, Uwepo wa Mungu ukidhihirishwa katika mtu huyu, hata wa—waliweka watu katika kivuli chake, nao waliponywa. Ni wangapi wanajua hilo ni la Kimaandiko? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hayo ni Maandiko tu kama Yohana 3:16 ilivyo. Unaona, yote ni Neno la Mungu. Sasa, watu, unajua kivuli cha mtu yule hakikuwaponya hao watu.

³⁵⁷ Lakini, angalia, kama nguvu za Mungu zilikuwa juu ya nabii huyo, kwa miaka na miaka baada ya Yeye kufa, hivi kwamba mtu aliyekufa alitupwa juu ya mwili wake, mifupa yake. Mwili hata haukuwapo; mifupa ilikuwapo. Na Uwepo wa

Mungu ulikuwa juu ya mifupa hiyo, mpaka mtu huyo aliyekuwa amekufa akafufuka.

358 Sasa hivi hamjui ya kwamba Mungu yule yule aliyefanya mambo hayo yote yuko papa hapa usiku wa leo? Kwa—kwangu mimi, nafikiri tunapaswa kuwa wenye furaha kuliko watu wote ulimwenguni kote. Wazia tu jambo hili.

359 Na—natumaini ya kwamba sijawafanya wasikilizaji wangu kuamini ya kwamba ni jambo fulani ninalofanya mimi mwenyewe. M—mnajua vizuri zaidi ya hivyo. Mimi, mimi ni ndugu yenu, mnaona, na mimi ni ndugu yenu tu.

360 Lakini ninajua, ninajua jambo hili, ya kwamba Mungu yuko hapa. Nami ninajua ya kwamba ametupa kitu fulani, ambacho hatuwezi kukielezea, ila kwa Neno la Mungu pekee, madai ya kwamba kinapaswa kuwa hapa wakati huu. Kwa hiyo, inatupa pia utambulisho kujua ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Inatupa utambulisho kujua ya kwamba watu hawa, hawa waliochaguliwa, walioteuliwa, walioitwa watoke, waliochaguliwa tangu zamani. . .

361 Sasa, hilo ni neno kubwa, *kuchaguliwa tangu zamani*, bali sote tunajua ya kwamba ni kweli. Tunajua kabisa kwamba Mungu asiye na kikomo aliyachagua tangu awali mambo yote kwa kujua Kwake tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, hata Mwana-Kondoo alichinjwa; na kila jina ambalo lingewahi kuwa kwenye Kitabu hicho, liliwekwa kwenye hicho Kitabu kabla Kitabu hicho hakijaandikwa. Sasa ni wangepi wanaojua hilo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

362 Naye Yesu alikuja ku—kuwakomboa wale waliokuwa katika Kitabu hicho. Katika Biblia, Mwana-Kondoo alikuja kutoka nyuma ya pazia, na akakitwaa kile Kitabu na kuifungua ile Mihuri iliyokuwa imekifunga, kwa kuwa Yeye alikuja kudai wale wote aliokuwa amewakomboa. Yeye ndiye Mwombezi sasa, Mwombezi akiwaombea hao aliokuwa amewakomboa. Wote ambao majina yao yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, wamekombolewa.

363 Kama vile nilivyofanya tamshi chungu na duni hivi majuzi usiku. . . Ninawangojea ninyi nyote mchukue leso hizi hapa. Sijaribu tu kurudia kuhubiri tena, bali nilisema kulikuwa na tamshi dogo. . . Natumaini jambo hili halisikiki la kukufuru, unaona. Lakini kama vile yule mkulima aliyeweka kuku aatamie, wala hakuwa na mayai ya kutosha, kwa hiyo akachukua yai la tai, naye akaliweka chini ya kuku naye akaangua tai. Naye alikuwa ni jamaa wa kipekee sana miongoni mwa hao kuku wote, kwa maana hawakuona mambo kwa mtazamo mmoja. Lakini huyo tu ndiye aliyewahi kumwona, ilikuwa ni huyo kuku. Yeye alisikia sauti moja tu, haikusikika kama ni sauti yake. Wala yeye asingeweza kutoa sauti kama ya

kuku au ya kifaranga cha kuku. Hakufurahia chakula chao, kwa kuwa wanakula kutoka kwenye eneo la boma. Kulikuwa na kitu fulani tofauti kumhusu yeye, hata hivyo hakujua kulikuwa na tofauti gani.

³⁶⁴ Na ndipo siku moja, kulikuwa na mama tai aliyejua ya kwamba alikuwa ametaga kiasi fulani cha mayai. Na kulikuwa na moja ya mayai hayo, ambalo lilikuwa liwe mwanawe, halikuwapo. Kwa hiyo akaenda kumtafuta, naye akamkuta katika boma la shambani. Ndipo akalia kwa sauti kuu. Na alipolia, maskini kifaranga hicho cha tai kilijua sauti ya mama yake. Kama vile Yesu alivyosema, “Kondoo wangu wanaijua Sauti Yangu.”

³⁶⁵ Nafikiri, jana usiku, wakati nilipoona hilo jopo la Wabaptisti, Wapresbiteri, na kadhalika, huenda walikuwa wameanguliwa chini ya kuku. Samahani, ndugu, unaona. Lakini Mama alijua alikuwa na wapenzi wake huko nje mahali fulani. Kwa hiyo hao watu waliokuwa wamesimama pale, wakiwa hawapingi mlo waliopata kutoka kwa mama kuku, na kadhalika, bali sasa wao ni tai, unaona, wanaruka kuendea chakula chao. Unaona?

³⁶⁶ Nami nafikiri kanisa ni kitu kama tamasha nililoona si muda mrefu uliopita, nikishuka kuja kutoka Tucson, ama kutoka—kutoka Phoenix, nikienda Tucson. Niliona tamasha la ajabu. Na kwa namna fulani lalinivunja moyo wangu, kuona kile kilichokuwa kimetendeka, jinsi...mwewe, aliyekuwa akiruka hewani, ndugu ya tai, ambaye ni mfano wa kanisa.

³⁶⁷ Naye Yehova ni Tai. Yeye aliwaita manabii wake “tai.” Yeye alijiita, Yehova, “Tai.”

³⁶⁸ Lakini huyu mwewe amepoteza utambulisho wake kwa muda mrefu, kwa maana haruki hewani tena na kuwinda chakula chake kama anavyopaswa kufanya. Bali yeye huketi juu ya waya za simu na kutenda kama ndege mla mizoga. Yeye—yeye huwinda sungura waliokufa ambao wameuawa na magari, naye pamoja na ndege wala mizoga wanatoka na kuenda huko nje na kula pamoja. Anarukaruka kama ndege mla mizoga, badala ya kutembea jinsi angepaswa kutembea. Yeye amepoteza utambulisho wake.

³⁶⁹ Nami ninasema jambo hili nikiwa na upendo wote wa kiungu na heshima, kwa muda mrefu kanisa limepoteza utambulisho wake kama dada tai. Linaketi hapo. Badala ya kuchimbua ndani ya Neno na kupata kujua kama mambo haya ni kweli, linangojea lundo la vitabu vya shule ya Jumapili ambavyo vimeandikwa na kundi la wasomi mahali fulani, sungura fulani aliyekufa ambaye ameuawa mahali pengine. Linarukaruka kama ndege mla mizoga! Mungu tusaidie kuruka kutoka kwenye mambo hayo.

370 Ahadi hizi ni kweli. Si vile mtu fulani alivyosema juu ya jambo Hilo, bali ni yale Mungu aliyosema juu yake! Ni za kweli. Nina furaha sana kuhusishwa na tai.

Hebu na tuombe pamoja kwa ajili ya wagonjwa wetu.

371 Baba mpenzi wa Mbinguni, imefundishwa katika Biblia ya kwamba walitoa kutoka katika mwili wa Paulo, lesa na aproni, na pepo wakawatoka watu, na pepo wachafu wakawaacha. Sasa, Baba, mimi nikisimama hapa juu ya lesa hizi, ninawakilisha kila mtu aliyepo. Ni mwili wa Kristo, sisi pamoja. Tunadai, kwa neema na upendo, ya kwamba tuko hapa kumwakilisha Bibi-arusi Wake, na tukiamini, tukishirikiana Naye katika Ufalme Wake. Nasi tunajua sisi si Mtakatifu Paulo, bali tunajua Wewe ungali ni Yesu.

372 Na tunaomba ya kwamba utaiheshimu imani ya watu hawa. Kama wangaliishi huko nyuma katika siku za Paulo, wangaliisikia Injili hii hii, wakaona mambo yaya haya. Kwa hiyo, hawa ni watu wa namna ile ile. Wewe ni Mungu yule yule. Kwa hiyo, ninaomba, Mungu mpenzi, ya kwamba utaiheshimu imani yao, kama ulivyowafanyia wale katika zile siku za Biblia. Na jalia kila nguvu za pepo, kila ugonjwa, kila mateso, ambayo yamewafunga watu ambao lesa hizi na vifurushi hivi hapa vinawakilisha, jalia nguvu hizo chafu za magonjwa ziwaache.

373 Ilisemwa, wakati mmoja, ya kwamba Israeli walikuwa wakitembea katika jukumu lao, kwenda katika nchi ya ahadi. Na wakiwa moja kwa moja katika jukumu lao, adui alikuja na kuwabana pembeni, nayo Bahari ya Shamu ikawazuia kutimiza jukumu lao, na katika safari yao. Ndipo Mungu akaangalia chini kutoka mbinguni, kupitia kwenye Nguzo ya Moto, ndipo bahari ikaogopa. Ilirudisha nyuma mawimbi yake, kwa maana mawimbi ya Mungu yalikuwa chini ya bahari. Nayo ikafanya njia kwa ajili ya watoto Wake, wakitembea katika utiifu.

374 Sasa, Mungu, kama Bahari ya Shamu iliogopa, na kutuliza mawimbi yake, kutuliza maji yake, na kuwapa nafasi watoto waliokuwa safarini wakitembea katika utii; Mungu Mpenzi, usiku wa leo, angalia kupitia Damu ya Mwanao, Yesu, Ambaye alitoa ahadi. Na wakati lesa hizi zitakapowekwa juu ya miili ya watu wagonjwa, naomba macho ya Mungu yaangalie, na jalia maradhi hayo, pepo huyo, aogope na kuondoka. Na jalia watu wadumishe safari ya kuelekea kwenye Nchi ya ahadi, wakiwa na afya nzuri na nguvu. Wakati Israeli walipotembea jangwani, hapakuwa na hata mtu mmoja mnyonge miongoni mwao, upande wa pili. Na wajalie watu hawa, Baba, kwa kuwa tunatuma lesa hizi, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

375 Mungu awabariki, kila mmoja. Mnapochukua lesa zenu sasa, aminini kwa moyo wenu wote. Je! mnaamini ya kwamba Mungu husikia haya? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Mimi, ninataka kusema jambo hili. Msininii, msitilie shaka, hata

kidogo. Unaona, linaweza kuonekana ni jambo la kigeni hakika. Samahani, hebu kidogo tu. Msitie shaka, hata kidogo. Lakini aminini sasa ya kwamba, tuliyoomba, Mungu atatujalia.

³⁷⁶ Je! mnaamini ya kwamba huyo ni Mungu hapa, anayejua siri ya moyo wako? Mnajua na mnaamini huyo ni Mungu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa kubali tu niani mwako sasa, haiwezi kuwa ni kitu kingine. Unaona?

³⁷⁷ Sasa, vipi kama kungekuwa na kesho iliyo ndefu, miaka mingi sana iliyopita jambo hili litakuwa ni historia. Na wakati watu, katika miaka ijayo, kama ingekuwa hivyo, watu wangukuja na kusema, “Vema, laiti ningalikuwa nikiishi wakati huo, ningeona jambo hilo likifanywa, jamani, hilo tu ndilo lingalililazimu kujua. Ningaliliamini jambo hilo papo hapo!” Unaona, jambo lile lile unaloamini, kama ungalikuwa kule nyuma wakati walipolifanya wakati huo! Kumbuka, ingali ni Yeye. Ni Uhai Wake ndani yako. Mungu awabariki. 

KUTHIBITISHA NENO LAKE SWA65-0426

(Proving His Word)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatatu jioni, tarehe 26 Aprili, 1965, kwa ajili ya mkutano wa Ushirika wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel katika Hoteli ya Embassy huko Los Angeles, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2010 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org